**BURUDANI** Uk. 20

## Ujuzi na vipaji ni fedha kubwa





**KIMATAIFA** Uk. 7

## UN: Mashambulizi ya Israel hayapungui Gaza



**MICHEZO** Uk. 24

## Simba bado haipo shwari




*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




## Mapinduzi ya kijeshi yalivyotikisa nchi za Afrika 2023


| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00044 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Desemba 27 - Januari 2, 2024 |


## Bilioni 5.3/- zahitajika kuirejesha upya Kilosa

Uk. 3




## Mchengerwa ataka watumishi kutekeleza miradi

Uk. 3



Uk. 5

## Askofu apigilia msumari ndoa za mashoga



## Makonda usiwaamshe wale waliolala

Uk. 12

**KITITA KIPYA CHA NHIF:**

# Wamiliki hospitali binafsi wamwangukia Rais Samia







Uk. 2

## Mabasi matano yapigwa 'stop' kusafirisha abiria

## Mrundikano kesi Kanda ya Dar wapungua

Uk. 2

# Mabasi matano yapigwa `stop' kusafirisha abiria

**Na Mwandishi**

JESHI la Polisi nchini, limeyazuia mabasi matano katika Kituo Kikuu cha Mabasi jijini Mbeya kuendelea na safari baada ya kukutwa na changamoto katika mifumo mbalimbali.

Akizungumza mapema jana, Mwanasheria Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Deus Sokoni, alisema baada ya kuendesha zoezi la ukaguzi wa mabasi, upimaji wa kilevi kwa madereva na utoaji wa elimu katika kituo hicho, jumla ya mabasi ya abiria 58 yamekaguliwa ambapo kati ya hayo matano yamekutwa yakiwa na changamoto mbalimbali.

Aliyataja mabasi hayo kuwa ni ya kampuni ya Turu Best, Isamilo Express, Arusha Express, Msigwa na Ahmed ambayo yalikutwa na hitilafu katika mifumo mbalimbali ikiwemo wa breki.

"Jeshi la Polisi nchini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kama vile Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), limepewa mamlaka ya kuzuia chombo cha moto kuendelea na safari pindi linapofanya ukaguzi na kugundua changamoto, ikiwemo ubovu na hitilafu katika mifumo ya chombo hicho," alisema Mrakibu Mwandamizi Sokoni.

Aidha, Afisa Leseni kutoka Latra, Amani Masuwe, alisema wamefanya jitihada kuhakikisha abiria waliokuwa wasafiri kwa mabasi hayo, wanapata usafiri mwingine na wengine kurudishiwa nauli zao ili kufanya utaratibu wa safari kwa siku nyingine.




## Mrundikano kesi Kanda ya Dar wapungua

**Na Mwandishi Wetu, Mahakama Kuu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, imewapongeza watumishi wake kwa kujituma kuchapa kazi na kuiwezesha kanda hiyo kupunguza mrundikano wa kesi 300 za muda mrefu ikiwamo za ugaidi zilizofanyiwa kazi mfululizo kati ya Oktoba na Desemba, mwaka huu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, Salma Maghimbi, alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na watumishi wa kanda hiyo alipokuwa akitoa salamu za Mwaka Mpya kwa watumishi hao.

"Ninawashuru sana pamoja na kwamba viongozi wengi tulikuwa wageni, lakini tumepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa watumishi na kuwezesha kwa kasi kubwa kufanya kazi kwa pamoja na kuitoa Kanda katika mzigo mkubwa wa mashauri hadi kufikia mashauri 50, hii ni hatua nzuri," alisema.

Aidha, aliwapongeza watumishi wote bila kujali kada kwa kuwa wote wameshiriki katika mafanikio hayo. Kwa sasa mrundikano wa mashauri ni chini ya 50 tofauti na ilivyokuwa awali.

Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, aliwasisitiza kuendeleza umoja, mshikamano na utendaji kazi mzuri kwa lengo la kuondoa mashauri ya mrundikano.

Kadhalika, alisisitiza matumizi ya mifumo mbalimbali iliyopo katika usikilizwaji wa mashauri ukiwemo mfumo wa e-CMS na wa Kunukuu na Kutafsiri (T.T.S).

Alieleza kuwa kwa sasa hakuna njia mbadala ya kuepuka mifumo hiyo zaidi ya kujifunza na kutatua changamoto chache zinazojitokeza ili kazi za kimahakama ziendelee kidijitali.

Aliwaahidi watumishi kuandaa mafunzo ya kujikumbusha kuhusu mpango mkakati wa mhimili huo na mifumo mingine ili kuwezesha kila mtumishi kushiriki kikamilifu katika kuutekeleza kwa mwaka 2024.

Alitumia kikao hicho kuwatakia heri watumishi wote katika sherehe za mwisho wa mwaka na mwaka mpya 2024.

Kwa mwaka huu, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, ilielekeza nguvu kubwa katika kuleta mabadiliko ya kifikra na kimtazamo, nguvu hizo ambazo pia zinatokana na watumishi, zimesaidia kuboresha utendaji kazi uliofanikisha kupunguza mashauri ya mrundikano.

Mahakama hiyo pia ilijiwekea malengo ya kuwa kituo bora cha mfano katika usimamizi wa shughuli za mashauri na kiutawala katika Mahakama ya Tanzania.



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, Salma Maghimbi

## Miaka 10 jela kwa kuua, kuiba

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mtaa wa Kineng'ene, Manispaa ya Lindi, Simoni Omari (30), amehukumiwa kifungo cha miaka 10 na miezi mitano kwa kosa la kumuua Mwanahawa Mandula (50).

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Rose Ebrahim wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Jaji Rose alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Nofard Setta, kama ana kumbukumbu ya makosa ya nyuma yaliyowahi kutendwa na mtuhumiwa ambapo alijibu kuwa hana, lakini akiiomba Mahakama impe mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Baada ya maelezo hayo, Wakili Issa Chiputula, aliyekuwa anamtetea mshtakiwa huyo, aliiomba Mahakama kumpunguzia adhabu mteja wake kwqa madai kwamba bado ni kijana na kwamba kukaa mahabusu kwa muda mrefu, kulimuathiri kisaikolojia na hakuisumbua Mahakama, hivyo anajutia kutenda kosa hilo.

Awali, ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali kwamba Aprili 13, mwaka 2021, katika eneo la Kinengene Halmashauri ya Lindi, mshtakiwa alimuua Mwanahawa Mandala, kwa kumpiga na silaha yenye ncha kali maeneo mbalimbali ya mwili wake.

**Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Jaji Rose alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Nofard Setta, kama ana kumbukumbu ya makosa ya nyuma yaliyowahi kutendwa na mtuhumiwa ambapo alijibu kuwa hana.**

# Bil. 5.3/- zahitajika kuirejesha upya Kilosa

**Na Mwandishi Wetu, Kilosa**



MKUU wa Wilaya Kilosa mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, amesema Sh. bilioni 5.3 zinahitajika kurejesha mazingira na hali za waathirika wa mafuriko, yaliyosababisha vifo vya watu watatu, kuathiri kaya 1,470, kubomoa nyumba 316 na nyingine 1,042 kuzingirwa na maji.

Shaka amesema miundombinu hiyo iliharibiwa na mafuriko yaliyotokea mwanzoni mwa Desemba, mwaka huu, maeneo mbalimbali wilayani humo.

Alisema hayo wakati akitoa taarifa ya tukio hilo kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliyefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa maagizo yake kwa watendaji kuhakikisha wanarejesha miundombinu ya wilaya hiyo.

"Mafuriko haya yalisababisha vifo vya watu watatu, yaliathiri kaya 1,470, kubomoa nyumba 316 na nyingine 1,042 kuzingirwa na maji pamoja na uharibifu wa ekari 303 za mashamba," alisema Mkuu wa Wilaya.

Alisema serikali ilitenga shule mbili kwa ajili ya kuwahifadhi waathirika waliokosa makazi hadi sasa, lakini bado wanahitaji mahitaji maalumu ikiwamo vyandarua na chakula.

Alitaja mahitaji mengine kuwa magodoro, dawa za kutibu maji, sabuni, nguo (mavazi) na mahitaji ya shule kwa watoto waliopotelewa na vifaa vyao katika tukio hilo.

# Mchengerwa ataka watumishi kutekeleza miradi ya Samia



**Na Hellen Mwango**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, amewataka watumishi wa wizara yake, kuhakikisha wanatekeleza miradi ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekasimisha mamlaka ya kuwatumikia wananchi katika maeneo yao.

Akizungumzia majukumu ya Tamisemi kwa mwaka 2023 kuwa yalilenga kutatua kero, changamoto mbalimbali katika jamii pamoja na kusogeza karibu huduma za kijamii kwa wananchi ikiwamo sekta ya afya, elimu na miundombinu.

"Nawapongeza watumishi wote walioko chini ya Tamisemi kwa kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia.

"Kwa upande wa elimu, shule za msingi 252 zimejengwa na kukamilika na shule za sekondari 444 zimejengwa maeneo mbalimbali nchini, nawapongeza watumishi wote wa umma kwa kusimamia na kutekeleza maelekezo hayo," alisema.

Alisema hayo juzi wakati akitoa salamu za Krismasi na Mwaka Mpya 2024 kwa niaba ya watumishi wa wizara yake, akiwashukuru na kuwatakia salamu hizo Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Mameya wote nchini, Wenyeviti wa Halmashauri na watumishi wote wa Tamisemi.

Aidha, aliwapongeza watumishi wote wa umma kwa kusimamia ujenzi wa zahanati, hospitali za wilaya kila mmoja wao atambue kazi zote wanazozifanya na kujitolea kwa ajili ya taifa.

"Tunampongeza Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi katika sekta ya afya, kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa jamii unaendelea kuimarika nchini," alisema.

Pia alisema Rais aliweka kipaumbele kwa watumishi wa umma katika kada mbalimbali zilizopo Tamisemi kufanikisha miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi, walimu, wahudumu na sekta ya afya ili watumishi hao wafanye kazi kwa furaha wakiwa na uhakika na makazi ya kuishi.

Waziri Mchengerwa alisema Rais Samia alitangaza elimu ya Tanzania kuwa bure kuanzia shule ya awali mpaka kidato cha sita, aliimarisha ujenzi wa miundombinu na kwamba kilichobaki ni jukumu la wazazi kuwaandikisha na kuwapeleka watoto shule.

Akitoa pongezi kwa walimu wote nchini kwa kazi kubwa ya 2023, alisema wanafanyakazi kubwa ya kuimarisha sekta ya elimu ya msingi kwa watoto kupata ufahamu wa kutosha katika kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Pia alichukua fursa hiyo kueleza kwa upande wa lugha ya Kiingereza kuwapongeza shule ya msingi na sekondari ikiwamo walimu darasa la tatu na kidato cha kwanza wanaojiandaa kuanza wiki sita za awali.

Aliwasihi na kuwaomba wazazi, walezi, walimu na viongozi wa serikali za mitaa kushirikiana kwa pamja kuwasiadia wanafunzi wa kidato cha kwanza kutambua uchaguzi wa masomo wanaokwenda kuanza kipindi cha wiki sita baada ya kuchaguliwa mapema mwezi ujao.

Vile vile, aliwapongeza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), kwa kazi kubwa walioyoifanya ikiwamo kuboresha miundombinu vijijini na mijini pamoja na kufunga taa za barabarani.

Aliwapongeza Tarura kwa kusimamia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inayowaelekeza ifikapo mwaka 2025, iwe imekamilisha miradi ya ujenzi wa barabara vijijini na mijini ikiwamo kufunga taa.

**KITITA KIPYA CHA NHIF:**

# Wamiliki hospitali binafsi wamwangukia Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**




WAMILIKI wa hospitali binafsi nchini, wamemwangukia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakimuomba kusitisha matumizi ya kitita kipya kilichotangazwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Wamedai kuwa kitita kipya kilichopangwa kuanza Januari mosi, mwakani, kitazichimbia kaburini hospitali binafsi kwa sababu zitapata hasara na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji.

Kwa mujibu wa taarifa yao, Rais Dk. Samia anajali sekta binafsi na wakati wote amekuwa akiwasisitiza viongozi wa serikali kushirikiana na sekta hiyo kupitia ubia maarufu kama PPP.

"Kwenye hili, hawajamwambia Rais, ukweli kwa sababu kitita cha mwisho kilikuwa mwaka 2016 na tangu wakati huo, hakijafanyiwa mapitio licha ya gharama za maisha kupanda, tumeendelea kutoa huduma katika mazingira hayo hayo magumu, lakini leo hii ghafla tena bila kutushirikisha, wanatangaza kushusha gharama.

"Sisi tunampongeza Rais Dk. Samia kwa kazi nzuri anayofanya tangu aingie madarakani na kwa dhati kabisa tumeona namna Rais wetu alivyo na nia ya dhati ya kuikuza na kuiendeleza sekta binafsi, lakini kuna watu hapa katikati wanafanya mambo ya ajabu kuikandamiza sekta hii, tunamuomba kwa hili, Mama Samia atunusuru.

"Kwa kuzingatia ukweli huu pamoja na mengine kama ucheleweshaji wa malipo kwa zaidi ya miezi minne, mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola kwa zaidi ya asilimia 20 ndani ya miaka saba, APHFTA tumeona tutashindwa kuwahudumia wanachama wa NHIF kama bei hizi zitaanza kutumika rasmi," ilisema.

Kwa mfano, taarifa hiyo ilisema, kushuka kwa gharama za kumuona daktari, upasuaji na kuchuja damu (dialysis), kutawafanya washindwe kumudu gharama halisi za kuhudumia wagonjwa wanaotibiwa kwao.

Ilisema bei za mwisho ziliwekwa tangu mwaka 2016 na tangu wakati huo, hazijawahi kufanyiwa mapitio licha ya gharama za maisha kupanda, sasa kushusha gharama kwa huduma ni sawa na kuzichimbia kaburi hospitali binafsi.

"Malipo yenyewe kwa watoa huduma yanaweza kukaa miezi hata sita hayajalipwa na wakati mwingine wanakataa baadhi ya madai ya malipo bila sababu za msingi, sasa haya yote hayajatatuliwa wanakuja kushusha gharama si wanataka kutuua," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa yao ilisema NHIF iliwaambia wafunge mfumo wa online kwa ajili ya kuwasilisha madai yao ya huduma wanazotoa ili wawe wanalipwa ndani ya siku 14 baada ya kuwasilisha madai hayo, lakini hali bado ni ile ile tangu wafunge.

"Tumefunga mfumo ambao umetugharimu Sh. milioni 80, lakini hizo siku 14 walizosema hawalipi na bado tunalazimika kusubiri miezi minne hadi sita, kama wanaona gharama za uendeshaji zimekuwa kubwa, wapunguze matumizi yao yasiyo ya lazima, lakini watibu watu," ilisema.

"Kwa hili, tunamuomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, atusaidie kwa sababu kwa hiki kitita ni kama wanataka kuzifunga hospitali binafsi, Rais wetu siku zote amekuwa akisisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi kupitia PPP, lakini hawa ni kama hawataki kuona tunajiendesha," ilisema.

Ilisema APHFTA iliwasilisha mapendekezo ya namna ya kuboresha uhai wa mfuko ikiwemo kuitaka NHIF ipitie upya mapendekezo ya kibiashara kwa bidhaa zake vikiwemo vifurushi vya `Wekeza, Timiza na Najali' na vinginevyo.

Ilisema walipendekeza NHIF itumie mfumo wa ukusanyaji madeni wenye ufanisi zaidi na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesababu za Serikali (CAG), ina maelezo ya kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakikusanywi na NHIF kwa taasisi nyingi.

"Kabla ya kutafuta suluhisho la nje, NHIF inapaswa kuonyesha msimamo wa kupunguza gharama za uendeshaji ndani ya mfuko na tukumbuke kwamba vituo vya afya, hospitali na NHIF wanategemeana kwaajili ya kuishi na kuwa endelevu hivyo hatupaswi kudhoofishana," ilisema

Ilisema kikao cha APHFTA kilikaa na kubaini kuwa baada ya ukaguzi wa madai ya Septemba, Oktoba na Novemba 2023 hospitali zote binafsi kuanzia ngazi ya Dispensari mpaka hospitali za rufaa zingepata hasara asilimia 25 kwa wastani.

"Na hii ni bila kuzingatia makato ya kila mwezi ukizingatia makato hayo yenye wastani wa asilimia 10 ambayo makato yenyewe yamejaa sintofahamu na utata mwingi yanafanya jumla ya hasara kufikia asilimia 35 kwa hospitali binafsi," ilisema

Wakati huo huo, wakati wakati APHFTA inadai kutoshirikishwa katika mchakato wa kushusha gharama, NHIF wamesema waliwashirikisha katika hatua zote.

Kwenye barua yake kwa hospitali mbalimbali za Mkoa wa Dar es Salaam, Meneja wa NHIF Mkoa wa Kinondoni, Dk. Christopher Lazeck alisema mwaka 2018 NHIF ilianza mchakato wa kuboresha kitita chake baada ya serikali kutoa mwongozo wa matibabu kwa lengo la kuwianisha huduma za kitita cha mafao, mwongozo huo na bei ya soko.

Alisema kupitia barua yenye kumbukumbu namba EA.35/269/01-A/32 kuhusu dhamira ya mfuko ya kuanza kutumika kwa kitita cha mafao kwa lengo la kupata maoni, NHIF ilikutana na wadau na kupata maoni mbalimbali kwaajili ya maboresho zaidi.

"Lengo la maboresho ya yaliyofanyika ni pamoja na kuhuisha kitita cha mafao na miongozo ya tiba nchini, kuweka usawa wa ada ya kumwona daktari bingwa kulingana na taaluma na ikama, kuboresha bei za huduma kulingana na hali halisi ya soko," alisema

Alisema maboresho yalilenga kuongeza motisha kwa watoa huduma vikiwemo vituo vya ngazi ya mkoa, wilaya na vituo vya afya na zahanati na kuwezesha huduma za kibingwa kupatikana karibu na wananchi.

**Kabla ya kutafuta suluhisho la nje, NHIF inapaswa kuonyesha msimamo wa kupunguza gharama za uendeshaji ndani ya mfuko na tukumbuke kwamba vituo vya afya, hospitali na NHIF wanategemeana kwaajili ya kuishi na kuwa endelevu hivyo hatupaswi kudhoofishana.**

# Askofu apigilia msumari ndoa za mashoga

**Na Mwandishi wa BBC**

ASKOFU wa Jimbo Katoliki Geita, Flavian Kassala, amesema hayuko tayari kubariki ndoa ya jinsia moja kwa kuwa ni kinyume cha maagano ya Mungu ya kutaka binadamu wakazaliane na kujaza ulimwengu.

Askofu Kassala aliweka msimamo huo alipokuwa akihubiri katika Misa ya Kitaifa ya Krisimasi iliyorushwa mubashara na Televisheni ya Taifa (TBC) juzi Jumatatu.

Alisema kubariki mapenzi ya jinsia moja, ni kwenda kinyume cha maandiko ya Mungu yanayotaka wanadamu wakazaliane na kuendeleza vizazi.

"Tumeingia kati hali ambayo tunabomoa hata njia za ujio wa watoto, mahusiano ya binadamu ambayo yanaondoa kabisa nafasi ya Mungu kuendeleza kazi ya uumbaji, wengine munayaita ndoa za jinsia, hakuna ndoa ya jinsia moja, ndoa ni moja tu, hata katika maangaiko yake, ni uhusiano wa mke na mume, binadamu na si binadamu na mnyama wa kiume au wa kike na kama tumeshindwa kuyatenda hayo kwa wanyama, imegeuka sasa kati yetu na kupiga kelele jambo hili lihalalishwe," alisisitiza Askofu Kassala.

Alisema binadamu anakataa uumbaji wa Mungu na kufanya mambo yaliyokatazwa huku wakitaka na Kanisa ibariki jambo ambalo amesema yeye hawezi kulifanya kamwe.

"Katika uchafu huo, sasa tunaomba tupewe na baraka, uje nikubariki katika hilo ambalo halina matumaini yoyote. Ni bora unaletee jiwe nitabariki ukajenge nyumba imara kuliko hali hiyo ambayo tunafikia sasa na kupigania na kuona ni haki," alisema " Askofu Kassala.

Desemba 18, mwaka huu, Vatican ilitoa waraka ulioidhinishwa na Papa Francis ukifafanua maana ya baraka, aina zake na utekelezaji.

Pia waraka huo uliruhusu Makasisi wa Kanisa Katoliki kuwabariki wapenzi wa jinsi moja.

Hata hivyo, Vatican ilisema kuwa kuwabariki wapenzi hao wa jinsia moja, haimaanishi kuwa ni kubariki ndoa za jinsia moja, bali baraka hiyo ni kwa watu wenyewe binafsi wenye uhitaji bila kujali hali zao za kiroho na kwamba ni jambo jepesi lisilozingatia uzito wa baraka za Kisakramenti au Kiliturjia.

Aidha, Vatican ilieleza pia kupitia waraka huo kuwa msimamo wa Kanisa Katoliki kuhusu ndoa, haujabadilika na kwamba ndoa ni muunganko kati ya mwanamume na mwanamke.

Hata hivyo, waraka huo ulipokewa kwa mitazamo tofauti hususan Barani Afrika, ambako Mabaraza ya Maaskofu Katoliki katika nchi za Nigeria, Zambia, Malawi na Madagascar, yalitoa nyaraka za kimaandishi kufafanua kwa waumini wao.

Mathalani, Baraza la Maaskofu la Zambia lilisema waraka wa Vatican kuwabariki wapenzi wa jinsia moja, halitekelezeki nchini huo kwani linakiuka mafundisho ya dini, mila desturi na sheria za nchi hiyo.

Kadhalika, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Yuda Theddeus Ruwa'ichi, alisema hawezi kuwabariki watu wawili wa jinsia moja wanaokwenda kwake.

Desemba 24, mwaka huu, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Nairobi, Kenya Philip Wanyolo, alitoa waraka unaokubaliana na msimamo wa Kanisa juu ya ndoa.

Lakini alipiga marufuku aina yoyote ya baraka ya makasisi wa jimbo hilo kwa uhusiano wowote usio rasmi au wapenzi wa jinsia moja akisema kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha Neno la Mungu, mafundisho ya Kanisa, utamaduni wa Kiafrika, sheria za mataifa na kwamba ni kashfa dhidi ya imani.

**Katika uchafu huo, sasa tunaomba tupewe na baraka, uje nikubariki katika hilo ambalo halina matumaini yoyote. Ni bora unilete jiwe nitabariki ukajenge nyumba imara kuliko hali hiyo ambayo tunafikia sasa na kupigania na kuona ni haki,"**


Askofu wa Jimbo la Geita, Flavian Kassala



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

## Ondoeni kero hii sokoni



SOKO la Stereo Temeke, ni kati ya masoko muhimu Dar es Salaam kutokana na watu wengi kupeleka bidhaa zao hapo. Lakini kero kubwa ni njia za soko hilo kuzibwa na wafanyabashara wanaopanga bidhaa zao chini hususani nyakati za asubuhi ambapo wafayabashara wengi wa magenge hufurika kutoka sehemu mbalimbali za Dar es Salaam kujipatia bidhaa.

Ukiwa sokoni hapo huku ukitembea kwa shida, mara unasikia kuli aliyebeba tenga la nyanya nyuma yako akija kasi akisema 'pisha, pisha hapo mbele'. Ni kawaida kuona watu wakisukumana, kuchafuana hadi kuanguka kutokana na ufinyu wa njia. Ni vema mamlaka husika zifanyie kezi.




## MAONI YA MHARIRI

# Wazazi tusilazimishwe na polisi kupeleka watoto shule

WATUMISHI wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wametakiwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu na miradi ambayo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekasimisha mamlaka kwao kwa ajili ya kuwatumikia wananchi katika maeneo yao.

Akitoa salamu za Krismasi na Mwaka Mpya, Waziri wa wizara hiyo, Mohamed Mchengerwa, kwa upande wa elimu, amesema Rais Samia aliamua kutoa elimu bila ada kuanzia shule ya awali mpaka kidato cha sita ili kuhakikisha wazazi hawapati uzito katika kupeleka watoto wao shule.

Sambamba na hilo, alisema Rais amekuwa akiimarisha ujenzi wa miundombinu ya shule nyingi nchini ikiwa ni pamoja na majengo, vyoo na vitabu.

Waziri pia alipongeza walimu wote nchini kwa kazi kubwa waliofanya katika mwaka huu unaomalizika, akisema wamefanya kazi kubwa ya kuimarisha sekta ya elimu ya msingi kwa watoto kupata ufahamu wa kutosha katika kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Pia Waziri amechukua fursa hiyo kuwahimiza na kuwapongeza walimu wa lugha ya Kiingereza wa shule za msingi na sekondari ikiwamo walimu wa darasa la tatu na kidato cha kwanza wanaojiandaa kuanza wiki sita za awali.

Akasema kilichobaki ni jukumu la wazazi kuwaandikisha watoto wa shule kuanza darasa la kwanza na wale waliofaulu mtihani wa darasa la saba kuanza kidato cha kwanza.

Hata hivyo, kumekuwepo na tatizo kubwa la wazazi katika baadhi ya maeneo ya nchi, kukataa kupeleka watoto wao shule, hususani wanaohitimu darasa la saba licha ya serikali kuwapunguzia sana uzito wa kusomesha watoto wao.

Uchunguzi umekuwa ukionesha kwamba wapo wazazi wanaokwepa kuwapeleka watoto wao shule kwa sababu kadhaa. Baadhi ya hizo ni ili wafanye biashara kuiongezea familia kipato, kufanya vibarua hususani kwenye mashamba mbalimbali, kushiriki shughuli za kifamilia kama kilimo au kuchunga mifugo na wengine kuolewa.

Kwa vile hali hiyo imekuwa ikienda kinyume cha Sheria ya Mtoto, walimu wakuu wamekuwa wakilazimika kutoa taarifa kwa mamlaka husika baada ya kuona watoto waliochaguliwa hawajiungi na shule zao. Hiyo imekuwa kisababisha wazazi kuanza kusakwa na askari wa mgambo au polisi ili kupeleka watoto wao shule.

Ni vyema tunapoelekea mwaka mpya, wazazi wasifikie huko.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com




Na Godfrey Sanga
Sangagodfrey26@gmail.com

## JICHO LANGU

# Sherehekea, andaa malengo 2024

NI vyema kwa kila mwanadamu anayeendelea kupumua kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa kibali cha kumaliza mwaka na hatimaye kujiandaa kuingia mwaka mpya. Wasanii fulani waliimba kwamba kumaliza mwaka salama si jambo rahisi sana!

Bila shaka ni haki husherehekea kuingia mwaka mpya kwa vifijo na bwembwe zikiambatana na vigelegele, vifijo na nderemo.

Lakini wakati tunaelekea kuumaliza huu mwaka wa 2023, ni vyema kila mmoja wetu ageuke nyuma na kutazama. Je, aliweka malengo na kama alijiwekea malengo, yametimia?

Umejiuliza ni kitu gani chanya kilichobadilika katika maisha yako ndani ya mwaka huu unaoisha au uliisha kuona jua linachomoza na kuzama?

Kwa uhakika ndani ya mwaka mpya, kitu kimoja tu huwa kinabadilika. Ni tarehe. Vitu vingine vyote hubaki kama vilivyo lakini kinachotakiwa ni wewe mwenyewe kubadilika!

Hivyo, ule usemi wa mwaka mpya na mambo mapya hayawezi kutokea na kubadilisha maisha yako endapo hutaanza kuweka mipango sasa. Kwanza unatakiwa wewe mwenyewe uwe tayari kubadilika unapoingia mwaka mpya.

Kati ya makosa ambayo unatakiwa kuyaepuka unapoingia mwaka mpya ni kutoweka malengo. Lakini malengo unayojiwekea, yawepo ya muda mfupi na ya muda mrefu pamoja na njia za kuyafikia. Usiweke malengo ya kufikirika zaidi.

Ni ukweli usiopingika kuwa mwaka unapoanza wengi huwa na matamanio ya kila aina lakini wanashindwa kuyatimiza kwa sababu ya kutokuwa makini katika kuorodhesha malengo yao.

> **Kati ya makosa ambayo unatakiwa kuyaepuka unapoingia mwaka mpya ni kutoweka malengo. Lakini malengo unayojiwekea, yawepo ya muda mfupi na ya muda mrefu pamoja na njia za kuyafikia. Usiweke malengo ya kufikirika zaidi.**

Baadhi ya vitu ambavyo wengi hubaki na matamanio lakini wakakosa malengo ya kutimiza ni pamoja na kufanya ibada, kufanya mazoezi ili kulinda afya ya miili yao na kujisomea vitabu ili kupata maarifa mapya ukiweka kando malengo ya kibiashara kwa maana ya kupanua uchumi.

Katika masuala ya uchumi, ushauri wangu ni kuzingatia kutokuwa na malengo mengi ndani ya mwaka mmoja na ambayo si rahisi kuyatimiza yote. Weka malengo machache lakini yanayotekelezeka.

Kumbuka mafanikio mara nyingi si rahisi na hayapatikani kwa siku moja. Kuna watu wanafikiri wakifanya kazi kwa juhudi kwa siku moja ya mwaka basi watafanikiwa kwa kiwango wanachotaka. Ukweli ni kwamba unapaswa kuweka juhudi kuanzia siku ya kwanza mpaka ya mwisho.

Haya ni baadhi ya mambo muhimu ambayo ukiyazingatia naamini yatakuongezea kitu katika ufahamu wako unapojipanga kuukaribisha mwaka mpya.

## VITA VYA ISRAEL, HAMAS:

# UN: Mashambulizi ya Israel hayapungui Gaza

**YERUSALEM, Israel**

MASHAMBULIZI ya anga ya Israel huko Gaza hayapungui, Afisa wa Umoja wa Mataifa (UN), ameiambia BBC, baada ya kutembelea hospitali inayotatizika kuwatibu majeruhi.

Gemma Connell, wa UN la kutoa misaada ya kibinadamu OCHA, aliiambia BBC kile alichokiona katika hospitali ya Al-Aqsa katikati mwa Gaza juzi Jumatatu kuwa ni mauaji kabisa.

Watu wengi waliojeruhiwa vibaya hawakutibiwa kwa sababu hospitali ilikuwa imejaa kabisa, alisema.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, hapo awali aliapa kuzidisha mapambano tena dhidi ya Hamas.

Netanyahu alisema alitembelea Gaza juzi Jumatatu asubuhi na kwamba operesheni ya kijeshi ya Israel huko haijakaribia kuisha.

Kauli yake inakuja siku chache baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, kusema Israel inapaswa kupunguza makali ya mashambulizi yake.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Ulinzi ya Marekani (Pentagon), imesema wanajeshi wa Marekani wamefanya mashambulizi ya anga nchini Iraq dhidi ya wanamgambo wanaodhaminiwa na Iran kujibu shambulio katika kambi ya wana anga ya Irbil na kuwajeruhi wanajeshi watatu wa Marekani, mmoja wao vibaya sana.

Waziri wa Ulinzi, Lloyd Austin, alisema mashambulizi hayo yalilenga vituo vitatu vinavyotumiwa na Hezbollah na washirika wake.

Alisema kumekuwa na mfululizo wa mashambulizi ya wanamgambo hao katika



kambi za Marekani nchini Iraq na Syria na kusisitiza kuwa Marekani haitasita kuwalinda watu wake na vituo vyake.

Kumekuwa na ongezeko la shughuli za Hezbollah na wanamgambo wengine wenye silaha katika eneo hilo baada ya operesheni ya kijeshi ya Israel huko Gaza. BBC.

# Mwili wa mama, wanawe wanne yakutwa ghorofani

**PARIS, Ufaransa**

WAENDESHA Mashitaka nchini Ufaransa, wameanzisha uchunguzi wa mauaji baada ya miili mitano kupatikana katika mji wa Kaskazini-Mashariki mwa Paris.

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya ndani, waathiriwa ni mwanamke na watoto wake wanne wadogo.

Miili yao ilipatikana katika mji wa Meaux ulioko zaidi ya kilomita 41 kutoka Mji Mkuu wa Ufaransa, Paris.

Waligunduliwa katika ghorofa, Mwendesha Mashtaka wa eneo hilo, aliliambia Shirika la Habari la Ufaransa la AFP.

Kulingana na tovuti ya habari ya Actu17, ambayo iliripoti kisa hicho kwa mara ya kwanza, polisi wanamsaka baba mwenye umri wa miaka 33, ambaye amekimbia.

Mwendesha Mashitaka, Jean-Baptiste Bladier, alithibitisha kwa vyombo vya habari vya Ufaransa kuwa Idara ya Polisi ya Versailles, ilikuwa ikichunguza. BBC.

# Ukraine yakanusha madai ya Urusi kuuteka mji muhimu

**KYIV, Ukraine**

RUNINGA ya taifa ya Urusi, ilionyesha majengo yaliyoharibiwa na wanajeshi wa Urusi katika kile ilichosema ni viunga vya Mariinka

Waziri wa Ulinzi wa Urusi, Sergei Shoigu, alisema wanajeshi wake wameuteka mji muhimu wa Mariinka Mashariki mwa Ukraine.

Hata hivyo, Kyiv imekanusha madai hayo. Shoigu alimwambia Rais Vladimir Putin, kwamba vitengo vya mashambulizi vimechukua



eneo lililoimarishwa sana nje kidogo ya Donetsk, Mji Mkuu wa eneo linaloshikiliwa na Urusi.

Lakini Msemaji wa Jeshi la Ukraine, Oleksandr Shtupun, alisema kupigania Mariinka kuliendelea.

Mariinka inayoonekana kama lango la kuingia Donetsk, karibu imeharibiwa kabisa.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Ulinzi ya Urusi ilithibitisha kwamba moja ya meli zake za kivita, ziliharibiwa katika shambulio la Ukraine dhidi ya bandari ya Feodosiya katika Jimbo la Crimea linalokaliwa kimabavu.

Mtu mmoja aliuawa, maafisa walisema. Mkuu wa Jeshi la Anga Ukraine, alisema ndege za kivita ziliharibu meli ya Novocherkassk iliyokuwa ikitua mapema jana.

BBC.



# Familia zisizojiweza kulipwa kila mwezi

**RABAT, Morocco**

MOROCCO imezindua mpango uliosubiriwa kwa muda mrefu wa kuzisaidia kaya maskini ambao unajumuisha malipo ya kila mwezi kwa karibu familia milioni moja zenye kipato kidogo nchini humo.

Tangazo hilo lilitolewa na Waziri Mkuu, Aziz Akhannouch, ambaye alisema wanufaika wa mpango huo watapokea kila mwezi kuanzia kiasi dirham 500 ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani 50.

Akhannouch alisema malipo ya kwanza chini ya mpango huo mpya wa taifa, yatafanyika kesho.

Mpango huo uliopendekezwa muongo mmoja uliopita ni sehemu ya mageuzi mapana ya utoaji huduma za jamii yaliyotangazwa na Mfalme Mohammed VI mwaka 2020.

Ajenda yake ya mageuzi ilijumuisha pia tangazo la mwaka 2021 la kuanza kutolewa bure kwa huduma za msingi za afya kwa raia wote wa Morocco. DW

# Ndege ya biashara ya binadamu yatua India

**NEW DELHI, India**

NDEGE iliyokuwa imewabeba mamia ya raia wa India waliokuwa wamezuiliwa kwa siku kadhaa kwenye uwanja wa ndege nchini Ufaransa kwa hofu ya ulanguzi wa binadamu imewasili nchini India.

Ndege ya kukodi ya Airbus A340, iliyokuwa ikisafiri kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwenda Nicaragua, ilizua shaka wakati wa kujaza mafuta.

Iliondoka ikiwa na abiria 276, lakini watu 25 wakiwemo watoto wawili, walisalia Ufaransa baada ya kuomba hifadhi.

Washukiwa wawili wa usafirishaji haramu wa binadamu, pia wamesalia nchini Ufaransa kwa uchunguzi zaidi.

Hata hivyo, wawili hao waliachiliwa huru na mahakama.

Ndege ya Legend Airlines ilitua Mumbai mapema jana kwa saa za huko.

Picha zilizochapishwa na Shirika la Habari la ANI, zinaonesha abiria kadhaa wakiwa wameketi kwenye viti vya plastiki kwenye uwanja wa ndege wa Mumbai baada ya ndege hiyo kutua.

Baadhi ya abiria walionekana wakitoka katika uwanja wa ndege, lakini BBC Idhaa ya Marathi, inaripoti kuwa wengi wao walikataa kujibu maswali kutoka kwa vyombo vya habari.

Ndege hiyo hapo awali ilikuwa imezuiwa kuondoka kwenye Uwanja wa Ndege wa Châlons-Vatry, yapata kilomita 130 kutoka Paris, Alhamisi iliyopita baada ya mamlaka kupokea taarifa isiyojulikana kwamba baadhi ya abiria wanaweza kuwa waathirika wa biashara haramu ya binadamu, Waendesha Mashitaka wa Paris walisema.

Wengi wa waliokuwemo ndani, waliaminika kuwa raia wa India wanaofanya kazi UAE.

Theluthi moja ya abiria wanaripotiwa kutoka katika Jimbo tajiri la Magharibi mwa India la Gujarat.

Mamlaka ya Ufaransa iliripotiwa pia kushuku kuwa huenda watu waliokuwa kwenye meli hiyo, walikuwa wakisafiri kwenda Nicaragua kabla ya kujaribu kuingia Marekani au Canada. Haijabainika iwapo mamlaka ilikuwa imeamua kwa uhakika kwamba hakuna uhalifu wowote uliokuwa umetendwa kabla ya kuruhusu ndege hiyo kuondoka.

Haijulikani pia kwa nini ndege hiyo ilikwenda Mumbai badala ya kuendelea na safari yake ya kwenda Nicaragua. BBC.






# Mapinduzi ya kijeshi yalivyotikisa nchi za Afrika 2023

**Na Mwandishi wa BBC**

KATIKA kipindi cha miaka minne (2020-2023), Bara la Afrika limeshuhudia mapinduzi kadhaa ya kijeshi hasa katika nchi za ukanda wa magharibi mwa bara hilo.

Nchi zilizokumbwa na mapinduzi hayo katika kipindi hicho ni Burkina Faso, Mali, Guinea, Niger na Gabon baada ya kipindi kirefu cha utulivu, ambao ulilisaidia bara la Afrika kuwa moja ya maeneo yaliyoshuhudia ukuaji wa kiuchumi na uwekezaji.

Kumekuwa na hisia mseto kuhusu hatua ya wanajeshi kuchukua mamlaka ya uongozi uliochaguliwa kwa njia ya kidemokrasia.

Wale wanaounga mkono hatua hiyo, wanasema ndiyo njia pekee ya kukomesha ukoloni mambo leo na wale wanaopinga wakisema inatishia amani, utulivu na maendeleo ya Afrika.

Tunapoelekea kukamilisha mwaka 2023, tunaangazia matukio makuu yaliyofanya nchi za kanda ya Afrika Magharibi kutawala vichwa vya habari.

## GABON

Agosti 30, mwaka huu, viongozi wa jeshi la nchi hiyo, walitangaza kumweka kizuizini Rais Ali Bongo, muda mfupi baada ya Tume ya Uchaguzi kumtangaza mshindi Rais huyo aliyekuwa akigombea muhula wa tatu madarakani.

Maofisa hao walijitokeza kwenye televisheni ya taifa na kutangaza kwamba wamechukua mamlaka, kufunga mipaka ya nchi hiyo na kuvunja taasisi zote za serikali.

Raia wa Gabon, walipiga kura Agost 26, mwaka huu kumchagua Rais, Wabunge pamoja na serikali za mitaa ambapo Ali Bongo, alikuwa akigombea Urais akimenyana na mpinzani wake, Albert Ossa.

Upinzani ulidai uchaguzi huo ulikumbwa na udanganyifu baada ya Bongo kutangazwa kuwa amepata asilimia 64 ya kura zilizopigwa.

Ushindi wa Bongo ungemfanya aendelee kuongoza nchi hiyo kwa muhula wa tatu wa miaka saba kulingana na Katiba ya nchi hiyo.

Kupinduliwa kwa Ali Bongo, kulitamatisha uongozi wa família yake uliyodumu kwa zaidi ya miaka 50 madarakani ambapo baba yake pekee Omar Bongo Ondimba, aliongoza kwa takriban miaka 42 kabala ya mwanaye kuchukuwa hatamu ya uongozi.

Ali Bongo aliingia madarakani mwaka 2009 baada ya kifo cha baba yake na kutawala kwa miaka 14 hadi uchaguzi uliofanyika Agosti 26 mwaka huu ambao ungemuweka madarakani hadi 2030.

## NIGER

Yalifanyika mapinduzi Julai 26, mwaka huu yakiongozwa na Jenerali Abdourahamane Tchiane.

Kuondolewa madarakani kwa Rais Mohamed Bazoum, kuliitumbukiza Afrika Magharibi katika mgogoro wa kikanda baada ya nchi jirani za Mali na Burkina Faso ambazo pia zilifanya mapinduzi ya kijeshi mwaka 2021 na 2022 mtawalio kuunga mkono hatua hiyo.

Tawala za kijeshi za nchi hizo zilionya kuwa uingiliaji wowote wa kijeshi dhidi ya viongozi wa mapinduzi ya Niger, utachukuliwa kuwa tangazo la vita dhidi ya Burkina Faso na Mali.

Duru zinaarifu kuwa kilichochochea mapinduzi nchini Niger ni mipango ya Bazoum kutaka kufumua uongozi wa juu wa jeshi na kumng'oa Jenerali Tchiani kutoka katika wadhfa wake wa Mkuu wa Majeshi.

Hiyo ni alama tosha kuwa mapinduzi hayo wala hayakuwa na nia ya kuirejeshea Niger mamlaka yake kamili ya kujitawala ama kuwakwamua wananchi kutoka kwenye umaskini bali kulinda maslahi ya maafande wakuu wa jeshi.

Rais Bazoum aliapishwa kuwa kiongozi wa Niger Aprili 2, mwaka 2021, akimrithi Mahamadou Issoufou, ambaye alikuwa ameongoza nchi hiyo kutoka 2011 hadi mwaka 2021.

Alikuwa mshirika wa karibu wa mataifa ya Magharibi na waangalizi wanaamini kuwa anazuiliwa nyumbani kwake katika Mji Mkuu wa Niamey.

Utawala wa Bazoum umeshirikiana na nchi za Ulaya katika jitihada za kujaribu kudhibiti wimbi la wahamiaji katika Bahari ya Mediterania.

Alikubali kurejesha mamia ya wahamiaji kutoka nchini Libya na pia kukabiliana na walanguzi wa binadamu katika vituo muhimu vya usafiri kati ya Afrika Magharibi na Kaskazini.

Baada ya utawala wa Bazoum kutimuliwa madarakani, mpango huo sasa huenda ukasambaratika.

## GUINEA

Mapinduzi ya kushtukiza ya kijeshi nchini Guinea, yalimaliza hatamu ya uongozi wa Rais Alpha Conde, uliokumbwa na utata, chini ya mwaka mmoja baada ya kushinda muhula wa tatu uliogubikwa na maandamano mabaya na ukandamizaji mkali dhidi ya upinzani katika taifa hilo la magharibi mwa Afrika.

Conde, mwenye umri wa miaka 83, alizuiliwa na wanajeshi wa kikosi maalum (GFS) Septemba 5, mwaka 2021, saa kadhaa baada ya ufyatulianaji wa risasi kuripotiwa karibu na makazi ya rais mjini Conakry.

Wakosoaji walihoji kuwa kiongozi huyo alifanya kazi kwa miongo kadhaa kurejesha demokrasia, lakini mara tu alipoingia madarakani, aliidhoofisha.

Kamanda wa GFS, Kanali Mahamady Doumbouya, alithibitisha kuchukua serikali kupitia runinga ya serikali na kuahidi kusimamia mabadiliko ya serikali kwa njia ya amani.

## BURKINA FASO

Chini ya miezi mitano baada ya wanajeshi kuonekana kwenye televisheni ya taifa nchini Guinea wakitangaza kuwa wamemuondoa madarakani Rais Alpha Condé, tukio hilo lilijirudia tena nchini Burkina Faso, huku jeshi likitangaza kupinduliwa kwa mkuu wa nchi, Roch Kaboré.

Chanzo cha uasi wa Jeshi la Burkina Faso, kama ilivyokuwa nchini Mali, ni mzozo wa usalama unaosababishwa na wanamgambo wenye itikadi kali ambao ulisababisha madhara makubwa.

Ripoti zisizokoma za mashambulizi ya wanamgambo zilichochea ghadhabu ya umma huku hisia za chuki zikiibuka miongoni mwa wanajeshi waliohisi wanatumwa nje, wakiwa na silaha nyepesi mno na kulipwa ujira mdogo au hata kupatiwa mlo kidogo, kuendeleza mapambano dhidi ya makundi ya wanamgambo.

## MALI

Mali imeshuhudia mapinduzi mawili ya kijeshi ndani ya mwaka mmoja (miezi tisa) baada ya Kanali Assimi Goïta, kumuondoa madarakani Rais Ibrahim Boubacar Keïta,Agosti mwaka 2020 na Rais wa Mpito, Bah Ndaw, Mei, mwaka 2021.

Raia wa Mali walikaribisha kutimuliwa kwa Keita, lakini utawala wa wanajeshi katika serikali hiyo ya mpito ulilaumiwa kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji wa mageuzi yaliyoahidiwa baada ya mapinduzi ya kwanza.

Baada ya kuchukua uongozi, Kanali Assimi Goïta, alisema Rais Bah Ndaw na Waziri Mkuu, Moctar Ouane, walishindwa kutekeleza majukumu yao na walikuwa na njama ya kuhujumu mchakato wa mpito nchini humo kwa kukiuka vifungu vya katiba viliyounda serikali mpito.

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

| Jumatano Desemba 27 - Januari 2, 2024 |

# Jungu kuu

KOLAMU

JAMII

SIASA



# Makonda usiwaamshe waliolala

UK. 12 & 13

Jamii




# Mvua za El-Nino na mafuriko yasiyotarajiwa, tumejifunza nini

**Na Dk. Felician Kilahama**

Moja ya vitu ambavyo viliumbwa na Mungu Mwenyezi ni dunia au 'sayari' kama inavyofahamika na wataalamu wa sayansi ya anga.

Maandiko Matakatifu yanatuthibishia kuwa Mungu, ndani ya siku sita, aliviumba vyote viijazavyo dunia ikiwemo binadamua. Baada ya kuona vyote alivyoviumba vimependeza na viko katika misingi imara kulingana na uumbaji alioufanya; siku ya saba akaitakasa (kwa Imani ya Kikristo), akapumzika lakini akatuamuru tuifurahie na kuitakasa.

Alituagiza siku sita tufanyekazi inavyotakiwa, na siku ya saba tupumzike na kumpa Mungu Utukufu, Yeye aliye Alfa na Omega .

Binadamu tuliumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, akatubariki, akatukabidhi mamlaka ya kuvimiliki na kuvitawala vyote vilivyoumbwa na Yeye.

Agizo tulilopewa na BWANA la kumiliki na kutawala vyote maanake nini? Kabla ya kulijibu swali hilo muhimu, niseme kuwa MUNGU aliyemuweza wa yote, ndiye Mamlaka Kuu na mwanzilishi wa sayansi ambayo inatumiwa na binadamu.

Yeye aliyafanya yote kwa ukamilifu wa hali ya juu sana. Kimsingi, wataalamu duniani tunajifunza kutokana na kazi aliyoifanya tangu kuwepo misingi ya dunia. Hivyo, tulipopewa mamlaka ya kumiliki na kutawala vyote; ilimaanisha tuvitumie kwa weledi mkubwa, tuyafanye yote kwa kiasi, bila uchoyo wala kuathiri uasilia wake (mother nature) na kuhakikisha katika kuvitumia tunaendeleza utukufu wake Mungu kupitia matokeo mazuri ya uumbaji wake.

Hebu tuuangalie Utukufu wa Mwenyezi Mungu kutokana na uumbaji alioufanya kwa kutumia NENO tu na vyote vikawepo katika ukamilifu wake. Yaani akitaka kuumba anatamka tu kitu fulani kiwe na kunakuwa. Hii pia imani ya Waislamu.o

Mwili wa binadamu ndio ulioumbwa tofauti na wanyama wengine hivyo kwa neema yake Mungu tunaishi. Kwa kuzingatia uumbaji wake Mungu, Tanzania Bara, ikawa kama ilivyo ni mfano halisi wa ukamilifu katika uumbaji.

Kutokana na uumbaji wa Mungu yafuatayo yanajitokeza: Sayansi ya Jiografia inaonesha kuwa Tanzania katika ujumla wake, kuna maeneo yenye milima kama Kilimanjaro, Meru, Livingstone au Uluguru pamoja na milima ya Pare Kaskazini na Kusini hadi kuelekea milima ya Usambara Magharibi na Mashariki ikiwemo iporoto 'ridges'.

Vilevile, kuna milima: Rubeho, Ukaguru, Nguu/Nguru, Malundwe, Mahenge, Udzungwa, Kitonga, Mpanga-Kipengere, Lukumburu, Kitulo, Sekenke na Nyango'ro. Hii ni baadhi, kiuhalisia kuna milima mingine Tanzania Bara pamoja na vilima vingi vilivyotawanyika sehemu mbalimbali nchini.

Kadhalika, kuna maeneo ya tambarale kama katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mwanza, Shinyanga na kwingineno. Vilevile, tunamiliki sehemu kubwa za Maziwa Makuu: Victoria, Tanganyika na Nyasa. Licha-ya hayo, kuna maziwa mengi kadhaa ndani ya nchi, mabwawa asilia na yaliyotengenezwa na binadamu mfano, Mtera, Kihansi, Kidatu, Mwalimu Julius Nyerere, na Nyumba ya Mungu na mengineo.

Vilevile, kuna mabonde karibu nchi nzima na miteremko mikali na ya kawaida. Yote haya yalitokana na uumbaji wa Mwenyezi Mungu katika mazingira tofautitofauti.

Tulipopata uhuru Disemba 9, 1961; karibu nchi nzima ilikuwa imefunikwa na uoto wa asili ikiwemo misitu minene, vichaka na nyasi, mbuga, mapori na ardhioevu na misitu-lindimaji.

Sehemu chache katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga zilikuwa wazi kutokana na kuondolewa uoto wa asili kwa sababu za kibinadamu ikiwemo kufukuza mbung o ili wasidhuru mifugo na binadamu.

Misitu ya asili, vichaka na mapori/mbuga na nyasi ni rasilimali inayochukua sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania. Faida zake ni nyingi, mojawapo yenye umuhimu sana, ni kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuhifadhi mazingira pamoja na kulinda vyanzo vya maji na ardhioevu (wetlands).

Kadhalika, Tanzania inamiliki sehemu ya Bahari ya Hindi ambayo tunanufaika kutokana na rasilimali zilizomo ndani yake na usafirishaji.

Katika kuyafanya hayo yote na mengineyo ambayo sijayataja hapa, pamoja na yaliyo juu angani na chini ya ardhi; Mwenyezi Mungu aliyafanya kwa ustadi mkubwa sana kiasi kwamba akili/ujuzi wa kibinadani haviwezi kufuadafu hata kidogo.

Tukichunguza kwa undani zaidi, yote yaliyomo ndani ya mipaka ya Tanzania; Mungu uliweka miundombinu ya asili muhimu. Kwanza, uotoasilia (misitu, nyasi na vichaka) husaidia maji ya mvua kuingia ardhini taratibu na hatimaye kufikia sehemu za chini ambako kuna mifumo ya asili ya mifereji ya kuyasafirisha maji chini ya ardhini mpaka kufikia sehemu zinazoruhusu maji yatokee nje hivyo kuanzisha chemichemi, vijito na mito. Misitu minene, ambayo ni misitulindimaji; hufunika milima na vilima hivyo husaidia kuhifadhi maji ya mvua kwa wingi na kuhakikisha udongo unakuwa salama nyakati zote.

Kazi ya vijito/mito ni kusafirisha maji kuyapeleka ziwani na/au baharini, mathalani, mito: Ruvuma, Rufiji, Ruaha-Mkuu, Kilombero na Kihansi. Pia kuna Ruvu, Wami na Zigi. Mito: Kagera na Mara, huingiza maji Ziwa Victoria na hutoka kupitia Mto Nile kwenda baharini.

Mungu Mwenyezi aliyafanya hivyo katika utimilifu wake pamoja na mifumo ya asili ikiwemo mabonde hatimaye miteremko/mifereji ya kusafirisha maji ya mvua na mengineyo na kuyapeleka yanapotakiwa kwenda hususani kwenye mito, maziwa, mabwawa na/au baharini.

Uwezeshaji na kufanikisha hivyo ni kazi aliyoikamilisha MUNGU kwa kuhakikisha kunakuwepo mazingira asilia ili kuepusha mafuriko au hali hatarishi kiasi cha kuathiri vibaya maisha ya wanadamu, wanyama na viumbe hai wengine pamoja na mimea/uoto asilia.

Hata hivyo, binadamu tumeongezeka maradufu kama Bwana alivyoagiza: zaeni muongezeke mukaijaze dunia (ingawa haijajaa).

Pamoja na kuongezeka, tumetokea kuwa waharibifu wakubwa wa mazingira asilia; ambayo Mungu aliyaweka katika misingi imara.

Tujiulize nini kilipelekea kuharibu mazingira kiasi cha kuhatarisha maisha yetu wenyewe? Siku hizi limekuwa jambo la kawaida kusikia mabadiliko ya tabianchi kuwa ndiyo chanzo kikuu kwa uharibifu wa mazingira hadi kuhatarisha uhai. Mathalani, mafuriko ya mara kwa mara au ukame usiotarajiwa kusababisha vifo kwa wanyama na watu pia.

Ni kweli, mabadiliko ya tabianchi yapo na yanaendelea kuwepo; lakini yote hayo ni matokeo mapana (athari hasi) kutokana na tabia/mitazamo/fikra na sera/maamuzi ya mataifa na binadamu sehemu mbalimbali duniani hadi kiasi cha kuhatarisha mazingira asilia kuwa kama yalivyo kote duniani.

Mabadiliko ya tabianchi kimsingi chanzo chake kikubwa ni ongezeko la joto duniani. Hii ni tangu mapinduzi ya viwanda yaliyojiri kati ya 1760 na 1840 katika Ulaya na Amerika; na mataifa husika kuanza kuondokana na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa mikono ya binadamu na kuanzisha viwanda vilivyochochea maendeleo na ustawi wa jamii hadi mataifa yenyewe.

Tangu wakati huo, kumekuwepo na ongezeko kubwa sana la kutengeneza bidhaa zinazohitajika kwenye masoko mengi duniani. Vyanzo vya nishati vikuu kwenye viwanda vikawa ni mafuta (industrial oil) na makaa ya mawe (coal). Kwa kiasi kikubwa vyanzo hivyo siyo rafiki kwa mazingira kutokana na kuzalisha gesiukaa ($CO_2$) ambayo ni kisababishi kikubwa kwa joto kuongezeka duniani hivyo kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

Kati ya karne ya 20 na 21 shughuli za viwanda zimepaa sana hivyo uzalishaji wa bidhaa unafanyika kwenye mabara yote duniani na kusababisha ongezeko kubwa la $CO_2$ angani; na huharibu ukanda za ozoni' hivyo kuruhusu mionzi ya jua kupenya kirahisi hadi kwenye ardhi na kusababisha joto kupanda.

Bara la Afrika linazalisha gesiukaa kwa viwango vya chini lakini shughuli za viwanda zinazidi kuongezeka hivyo uwezekano wa kuzalisha $CO_2$ nyingi ni mkubwa labda jitihada makusudi zitumike kuongeza matumizi ya nishati iliyo rafiki kwa mazingiara kama umeme unaotokana na nguvu za maji (hydroelectricity) au unaotokana na gesiasilia na nguvu za jua (solar); jotoardhi (geothermal) na nguvu za upepo.

Kwa upande mwingine, Tanzania, tunachangia gesiukaa angani kwa kufyeka misitu/mapori na kuichoma moto hovyo. Isitoshe, kilimo na ufugaji nchini havijawa rafiki kwa utunzaji wa mazingira; wakulima na wafugaji hufyeka misitu/mapori bila kujali athari zake kwa mazingira.

Ingawa wanafanya hivyo kwa nia njema ya kulima au kupata chakula pamoja na mazao ya biashara; ila matokeo yake ni hasi kwa mazingira. Vivyohivyo, kwa wafugaji wanapochoma moto kupata nyasi kulisha mifugo au kufukuza mbung o wasidhuru mifugo yao wanasababisha tatizo la kimazingira.

*Itaendelea.*



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Filamu za kigeni, vitabu vya nje na malezi ya kizungu

KUTOKANA na harakati za kufukuzana na maisha pamoja na kutenga muda kwa ajili ya ibada, mazoezi na kujisomea, nimekuwa sipati muda mzuri sana wa kuangalia michezo ya kuigiza kwenye runinga. Hivyo huwa ninaangalia mara mojamoja.

Miezi kadhaa nyuma kama si mwaka, nilipokuwa nina mpango wa kuandika mchezo wa kuigiza kutokana na moja ya riwaya zangu, nililazimika kuangalia mchezo mmoja uliopewa jina la The City ili nione kana kuna cha kujifunza.

The City ulikuwa mchezo mzuri, na moja ya kitu nilichojifunza katika mchezo huo ni watayarishaji kuja na mchezo ambao sehemu kubwa ya mikasa au visa vinafanyikia katika nyumba moja na hivyo kuokoa bajeti kwa kupunguza matumizi ya nyumba nyingi! Hongera sana mtunzi.

Tofauti na waangaliaji wengine, mimi unaweza kunikuta naangalia filamu, lakini nikawa sizingatii kabisa kisa kinasema nini bali kuangalia upigaji wa picha unavyofanyika, uvaaji wa uhusika, makosa, utamaduni wao kulinganisha na wetu (kwa michezo ya nje) yakiwemo mavazi na mengine mfano wa hayo.

Katika mchezo huo wa The City na mwingine niliouangalia hivi karibuni japo si wote katika kituo cha Azam (Unfaithful), kuna mambo kadhaa niliyaona yakuwa na ukakasi, mintarafu kama utazingatia utamaduni wetu.

### MTOTO KUMGOMBEZA MZAZI

Moja ya ukakasi lilikuwa ni suala la heshima ya watoto kwa wazazi wao. Si kwamba katika michezo hiyo wazazi hawaheshimiki lakini nilishuhudia katika baadhi ya mazingira, watoto wakidekezwa sana na wakati mwingine kuwaijia juu wazazi wao mithili ya kuwagombeza!

Sisemi kwamba wazazi wanapaswa kuwa madikteta kwa watoto wao au kutowapa demokrasia ya kueleza hisia zao lakini kwa tamaduni zetu kama Waafrika, sharti mtoto awe na mipaka anapoongea na mzazi wake.

Katika mila zetu, hata kama mzazi ndiye kakosea mtoto hawezi kumgombeza, bali atatumia lugha ya upole na staha kueleza hoja zake.

Pale jirani yangu 'Uswazini' kuna binti mmoja hana adabu kabisa kwa mama yake mzazi. Kumbwatukia, kumsema vibaya kwa watu baki kama sisi ni jambo la kawaida kabisa kwake.

Kupitia filamu hizo mbili, nimehisi tatizo la huyu binti lilipoanzia. Tangu nimeanza kumfahamu akiwa binti mdogo, ni mpenzi mkubwa wa kuangalia michezo ya kuigiza ya nje kwenye runinga hadi usiku wa manane!

Ninahisi huko ndiko amezoa 'haki na sababu' ya kumbwatukia mzazi wake!

### KWENYE VITABU NAKO

Kupitia mitandao ya kijamii, hivi karibuni nimemsikia bwana mmoja, mkazi wa Mombasa, Kenya, akihofu kutokea kwa athari hasi miongoni mwa vijana kufuatia ujio wa meli inayoitwa Logos jijini Mombasa, inayoelezwa kuwa ni maktaba inayoelea, kubwa kuliko zote duniani.

"Hizi meli msidhani zinakuja bure, wana ajenda zao. Lakini hakuna viongozi wa dini zetu waliokwenda pale (kuangalia athari za maadili) lakini mjue vijana wetu walikwenda pale (kwa wingi)."

Anasema yeye alikwenda kwa jicho la udadisi kutaka kujua ni vitabu gani vipo katika maktaba hiyo inayoelea, vinahusu nini na vimeandikwa na nani.

Bwana huyo anasema cha kwanza alichogundua maktaba ile ina ubaguzi wa dini. Hakuona vitabu vinavyozungumzia dini yake ya Kiislamu hata kimoja ingawa asilimia kubwa ya wakazi wa Mombasa ni Waislamu!

Lakini kubwa anasema vitabu vingi alivyopitia vinafundisha maisha na malezi ya kizungu. Siku hizi ukisikia mtu akisema malezi ya kizungu anamaanisha hata haya yanayopigiwa debe na wazungu ya kuheshimu na kutambua mapenzi ya jinsia moja!

Kwamba mapenzi ya jinsia moja ni haki lakini ndoa za mitara ni unyanyasaji!

"Vitabu (nilivyoona kwenye hiyo meli) vinazungumzia namna gani msichana au mvulana alelewe kizungu... Sikatai watu kuingia pale kupata maarifa ya kwenye vitabu lakini ni mafundisho yapi wanapata hasa?" Anasema huyo bwana kwenye hiyo klipu.

Anasema katika uchunguzi wake, aligundua hata walimu waliokwenda pale na wanafunzi, hawakuchunguza kujua malengo ya wazungu wale na kuwasimamia vyema wanafunzi kuhusu aina ya vitabu wanavyopaswa kusoma.

### TUCHUKUE TAHADHARI

Nimeandika haya ili kuwakumbusha wazazi, taasisi mbalimbali, jamii kwa ujumla na hata serikali kuwa makini na michezo ya kigeni tunayotafisiriwa na hata vitabu kutoka nje.

Wanaotafisiri michezo hii, pia waondoe kila chenye ukakasi kwa mujibu wa mila zetu kama Waafrika.

Wazungu, baada ya 'kuharibu' tamaduni zao ni kama wanaudhika kuona sisi Waafrika bado tuko vizuri, tamaduni zetu nyingi zikiendana na maandiko ya vitabu vitakatifu, hivyo wanatamani kuona na sisi 'tunaharibikiwa' kama wao!

Na hii ni hulka ya mwanadamu yeyote. Mchagga, kwa mfano, angetamani dunia nzima wawe Wachagga na kipindi hiki cha mwisho wa mwaka wawe likizo Kilimanjaro wakichoma nyama. Vivyo hivyo kwa Mhaya, Msukuma na kadhalika.

Muislamu halikadhalika angetamani watu wote wawe Waislamu, wazungu pia wanatamani tufuate maadili yao waliojitengenezea kwa kisingizio cha kwenda na wakati, haki za bindamu au uhuru wa mtu!

Ninajua tunaishi katika zama mgumu za utandawazi, zama ambazo dunia ni kijiji. Kinachofanyika sasa hivi Ujerumani unakiona kama si kukisikia ukiwa Tanzania.

Lakini yale mabaya, yanayokwenda kinyume na tamaduni na imani zetu za kidini na ambayo tunayoweza kuyaepuka hatuna budi kufanya hivyo. Kwa mfano, katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza tunapaswa kuendelea kuachana taratibu na michezo ya nje na kujikita kwenye michezo ya ndani, iliyotungwa kwa kuzingatia maadili na uasili wetu.

Nikisema uasili namaanisha kitu kama hiki: Niliwahi kuangalia filamu moja ya Kibongobongo, bastola zikwa zinatembea njenje hadi muuza chipsi anayo! Mbali na filamu hiyo kufundisha ukatili na ubabe, nikawa najiuliza hii ni Tanzania gani ambayo kila mtu anamiliki bastola! Mbali na kuhisi ukakasi, nisingeshangaa sana kama ingekuwa watu hao wanachimana visu au kukatana mapanga!

Tanzania ninayoijua mimi ukisikia bastola basi ni askari, mfanyabishara mkubwa au jambazi, lakini muuza chipsi! Labda kama nimepitwa na wakati.

Ninaandika ili ikiwezekana tufute kile ambacho nimezoea kusikia watu wakisema: "Siwezi kupoteza muda wangu kuangalia filamu/maigizo ya kibongo."

Mbali na makosa mengi katika filamu zetu kama ya kukosa mwongozo mzuri (screenplay), uongozaji uliokwenda shule (directing), uchaguzi wa hovyo wa washiriki, uzalishaji wa viwango vya chini (hii mara nyingi ni kutokana na ufinyu wa bajeti) na kadhalika na kadhalika, tatizo lingine limekuwa ni hadithi zisizovutia na zisizozingatia utamaduni na mazingira ya Tanzania.

Ndio maana katika makala mbili zilizotangulia pamoja na hii, ninaendelea kuhimiza watayarishaji wetu wa filamu kushirikiana na waandishi wa riwaya, pengine tukapunguza tatizo la kupata filamu zenye hadithi zisizovutia au zisizongatia maadili na uasili wetu.

> **Vitabu (nilivyoona kwenye hiyo meli) vinazungumzia namna gani msichana au mvulana alelewe kizungu... Sikatai watu kuingia pale kupata maarifa ya kwenye vitabu lakini ni mafundisho yapi wanapata hasa?**

### MBONA SOKA LIKO JUU?

Kwa kutumia mfano wa soka, kumbukumbu zangu zinaonesha kwamba miaka michache tu iliyopita, Watanzania walipendelea kuangalia zaidi soka la nje, hasa ligi ya Uingereza kwa sababu walikuwa wanaona ladha kuangalia mpira safi kuliko soka letu la kubutuabutua.

Lakini maboresho ambayo yamefanywa na vilabu vyetu kutokana na uwekezaji mkubwa, soka la ndani sasa linavutia wengi. Hata juzi wakati ikielezwa kwamba ligi inaahirishwa, nimesikia watu wakisikitika kwamba watakaa muda mrefu bila kuona burudani ya boli.

Filamu zetu ambazo ni kiwanda adhimu cha kutengeneza pesa na ajira, zinaweza kuvutia pia uwekezaji mkubwa kama umakini utazidi kutawala.

Lakini ni vyema pia wadau, taasisi mbalimbali na serikali kuendelea kuhimiza uandishi wa vitabu vikiwemo vya malezi na vya watoto, vya Kiswahili na Kiingereza.

Naipongeza serikali kuanzisha Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ambayo inaleta chachu ya Watanzania kuandika riwaya, mashairi na vitabu vya watoto lakini natamani kuona taasisi nyingine pia zikijitokeza kutoa tuzo kwa lengo hilohilo.

Wadau, wazazi na walimu pia wana dhima ya kuhimiza usomaji wa vitabu kwa watoto, tena vya waandishi wa Afrika, ili kuepuka watoto wetu kusoma zaidi vitabu vinavyofundisha malezi ya kizungu yakiwemo matendo yaliyolaaniwa ya ushoga.

Siasa

# Makonda usiwaamshe waliolala

## ■ Wapinzani wanasubiri chaguzi waibuke na UDETA, UKAWA



Na Hamid Yassin

WAHENGA walinena kuwa, ukimwamsha aliyelala, utalala wewe!

Nimemsikia Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda akisema alipunguza kasi ya kukipigia debe chama chake hivi karibuni kwa sababu wapinzani wao hawaonekani kwenye uga wa siasa!

Bila shaka ni kweli viongozi wengi wa vyama vya upinzani wamelala usingizi wa pono, lakini hali hiyo haitakiwi kumfanya Makonda na makada wenzake wa chama tawala kinachoendelea kutuunganisha Watanzania na kudumisha amani tuliyo nayo abweteke, kwani hiyo ni kawaida yao.

Tangu kuanza kwa mfumo huu wa vyama vingi mwaka 1992 hakuna chama cha upinzani kimewahi kufanya siasa japo kwa miaka miwili mfululizo!

Miaka sita ya uongozi wa Awamu ya Tano chini ya hayati John Pombe Magufuli angalau vyama vya siasa vya upinzani vilipata mwamvuli wa kujifichia kwamba vimezuiwa kufanya harakati za siasa baada ya kumalizika kwa uchaguzi, lakini ukweli ulio dhahiri vilikuwa vinacheka 'jino pembe' kwani hiyo ni kawaida yao!

Daima vyama hivi huibuka na kujaribu kufanya siasa nyakati za kuelekea chaguzi mbalimbali au wakati wa matukio wanayoona wanaweza kuyageuza fursa ya kukinyooshea kidole CCM na Serikali yake!

**WAPI SERA MBADALA**

Yaani ni vyama ambavyo vimekuwa vikisubiri CCM na Serikali wafanye makosa ya kibinadamu vipate cha kusema badala ya muda wote kueleza sera mbadala.

Kwamba vingekuwa vikisufia hata mazuri yanayofanywa na CCM kisha kueleza namna ambavyo labda wangefanya vizuri zaidi kama wangekuwa wao!

"Watu wanahoji mbona sionekeni majukwaani au sisikiki, sasa nijitokeze hadharani kujibu au kuongea nini huku wapinzani wenyewe hawafanyi hata mikutano ya hadhara wakati wameruhusiwa na kuhakikishiwa ulinzi?" Aliuliza Makonda kwenye mkutano wake na waandishi wa habari wiki iliyopita.

Hata hivyo, nilifurahi kumsikia Makonda kwenye mkutano huo huo na waandishi baadaye akisema kwamba anajiandaa kufanya ziara kwenye mikoa kumi ili kuendelea na zoezi la kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusikiliza kero za wananchi.

Hapo safi, hivi ndivyo anavyotakiwa kufanya kwa mtazamo wangu, lakini akisubiri kwanza wapinzani wafanye nini au watamke kipi ili awajibu, itakula kwake katika kipindi kama hiki, kwani uzoefu unaonyesha hata hao wapinzani, kama nilivyodokeza, agenda zao kuu hutokana na matukio au matamko ya CCM!

Vipo vyama vya upinzani vile vinavyochukuliwa kama vidogo ama visivyo na nguvu ya ushindani ambavyo havipati hata ruzuku ya kujiendesha kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, hivi unaweza kuwaelewa viongozi wao wanaposema hawana fedha ya kumudu kufanya siasa ya kuzunguka

Siasa



nchi nzima kujiimarisha ama kujinadi kwa wananchi ili kujua sera zao.

Lakini hivi vinavyoitwa vyama vikuu vya upinzani hawana kisingizio chochote cha kutofanya siasa za maana mbele ya wananchi. Kazi yao narudia kusema imekuwa ni kusubiri matukio wanayoona yanaweza kuwa faida kwao kisiasa na kuwachochea wananchi mbele ya serikali yao!

Mfano ni hili suala la kuhamishwa kwa hiari kwa wakazi wa Ngorongoro ili kuboresha hifadhi hiyo ambayo iko hatarini kutoweka lakini kuna chama cha siasa imelivalia 'kibwaya' hadi kulifikisha Bunge la Ulaya wakidai eti haki za binadamu zinavunjwa huku Tanzania!

**MUDA WA KUTOKA USINGIZINI**

Zimebaki siku chache kabla ya kuingia mwaka 2024 ambao utakuwa na chaguzi za serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, hapo sasa Makonda ndiyo ataviona hata vile vyama vilivyolala usingizi wa pono kwenye ulingo wa siasa vikikurupuka kusaka 'huruma' ya wananchi!

Lakini bahati mbaya kwao, kamwe haviwezi kufurukuta vitakutana na wajanja toka vyama dume vya upinzani na kuanza kuimbiwa yale mapambio yaliyozoeleka ya 'UMOJA' wa wapinzani zinapofika nyakati hizo za chaguzi!

Huu ndiyo wakati ambao wajanja toka vyama kama kile cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), NCCR- Mageuzi, Chama cha Wananchi (CUF) na siku hizi ACT Wazalendo huibuka na kuanza kuimba ngonjera za kuunganisha nguvu ya kuing'oa CCM madarakani!

**UKAWA KUFUFUKA?**

Makonda sasa atasikia ule Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ukifufuliwa hata kwa jina lingine huku ulaghai wa kuachiana majimbo kwenye hizo chaguzi ukiimbwa kwa sauti ya ndege mnana!

UKAWA ambao ulianzishwa na vyama vya Chadema, CUF, NCCR- Mageuzi na NLD wakati ule wa Bunge la Katiba na kisha kuhamishiwa hadi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 na baadaye ule Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, uliishia kuwa shubiri miongoni mwa viongozi wa vyama hivyo na wanachama wao.

Nakumbuka kupitia gazeti moja kubwa hapa nchini la tarehe 24 Machi 2015 lilimnukuu Katibu Mkuu wa NCCR Mageuzi (wakati huo) akilalamikia kuwa hawatakubali UKAWA utumike kwa maslahi ya chama kimoja katika umoja huo. Kauli ile ilikuwa ni ishara kwamba hali haikuwa shwari ndani ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Katibu Mkuu yule wa NCCR Mageuzi alitanababahisha kwamba viongozi wao wa juu walikuwa wazito kusema ukweli wa mambo kuhusu kilichoendelea ndani ya UKAWA.

Baadaye akaibuka kiongozi wa Kitengo cha Vijana wa chama hicho, Deo Meck ambaye pia alipinga umoja ule wa mashaka wa UKAWA na kusisitiza Chadema ilikuwa na lengo baya dhidi ya vyama vingine vilivyounda umoja ule.

**ILIANZA UDETA**

UKAWA haukuwa umoja wa kwanza wa wapinzani kama nilivyoandika hapo juu, vyama vya upinzani huwa vinaibuka nyakati za chaguzi tu na baada ya hapo vinapotea ama kugeuzwa kuwa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO) za viongozi wajanja kutafuta na kupiga fedha kimya kimya!

Baada ya upinzani kugaragazwa na CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, mwaka 2006 uliundwa ushirikiano wa vyama vya siasa Tanzania uliojulikana kama Umoja wa Demokrasia Tanzania (UDETA), ukishirikisha Chama Cha Wananchi (CUF), wakati huo kikiwa chama kikuu cha Upinzani Tanzania, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), NCCR-Mageuzi, na Tanzania Labor Party (TLP).

Dhamira ilikuwa ni kujenga upinzani imara kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Kama ilivyo ada umoja ule ulikufa muda mfupi tu toka kuanzishwa kwake kutokana na dhamira ovu ya baadhi ya vyama hivyo, hususani Chadema ambavyo malengo yake yao yalikuwa ni kujijenga kupitia migongo ya vyama hivyo.

Kwa mfano, katika ziara za mikoani zilizofanywa na viongozi wa vyama hivyo, Chadema walichukua mawasiliano na viongozi wa vyama vingine na baadaye kuwashawishi kujiunga na chama hicho.

Hila hizo na ulaghai huo ulipelekea UDETA kufa kifo cha kawaida bila hata kikao cha kuamua kusitisha umoja huo.

Ikumbukwe mwaka 2010 Chadema baada ya kupata wabunge wengi ilibeza vyama vingine kwa kuviita CCM B ama vyama mamluki wa CCM na kwamba isingeweza kushirikiana navyo. Ikasahau jinsi chama cha wananchi CUF kilivyowaalika na kuwapa vyeo katika muda ambao kilikuwa na uwezo wa kuunda kambi rasmi ya upinzani pekee Bungeni.

Ilipoundwa UKAWA baadhi ya vyama vilitegemea kwamba viongozi wa Chadema kwa wakati ule wangekuwa wamejifunza na kwamba wangebadilika na kufanya siasa za kistaarabu zinazozingatia maslahi ya nchi na watu wake na washirika wenza wa UKAWA, lakini wapi, waliwafanyia uhuni kuliko hata ule wa wakati wa UDETA.

CHADEMA ndani ya UKAWA mtiririko wa matendo yake ulionesha kwamba chama hiki kilikuwa bado ni kilekile na nia yake ilikuwa ni kutumia vyama vingine katika kuficha udhaifu wao na kujipatia maslahi ya kisiasa dhidi ya vyama hivyo vilivyounda umoja ule.

Nitatoa mifano michache. Wakati wa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014, UKAWA ulitengeneza dokezo moja kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa. Lakini nyuma ya pazia, Chadema wakatengeneza dokezo lao na kuwapa viongozi wao maelekezo kuhakikisha kuwa kila sehemu lazima waweke wagombea.

Wakati vyama vingine vilifuata mwongozo wa UKAWA, Chadema wakawa na maelekezo yao tofauti, na zaidi ya hapo walienda mbali na kuwaeleza wagombea wa vyama shirika wanaokubalika kujaza fomu za chama hicho maana ndiyo umoja huohuo!

Hali hiyo ya kucheza faulo, na mwamko ule wa wananchi kuchagua umoja huo, kwa kuwa Chadema waliweka wagombea wengi mwisho wa siku wakapata viti vingi na viti hivyo wakaja kushinikiza viwe vigezo vya uteuzi wa wagombea ubunge 2015.

Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, aliachiwa jimbo na chama cha wananchi CUF, tena nje ya kikao, kwa utashi wao na kwa nia ya kudumisha mahusiano. Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kwamba Makamu Mwenyekiti wa NCCR - Mageuzi aliyegombea urais Zanzibar mwaka 2010, na aliyekuwa moja ya nguzo za kuasisiwa kwa UKAWA, hakupewa nafasi ya kuachiwa jimbo hata moja kule Zanzibar.

Swali la kujiuliza lilikuwaje mtu ambaye ndiyo kwanza alitoka kuingia katika harakati za kisiasa anapewa nafasi ya kugombea lakini viongozi wa NCCR-Mageuzi wazoefu hawakupewa hiyo fursa?

Ile ilikuwa moja ya sababu ya kuyumba kwa UKAWA, kwani vijana wa NCCR-Mageuzi waliona kwamba hali ile ina kasoro na iliyohitaji isemwe, maana kulikuwa na walakini katika maamuzi yote yale.

Maswali mengine ya kujiuliza ilikuwa kama Naibu Katibu Mkuu Chadema, ambaye hakuwa na mizizi wala chembe ya siasa kule Zanzibar anaachiwa jimbo, je ni kwa nini ilikuwa shida kuliacha jimbo la Serengeti kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi ambaye alikuwa na historia ndefu katika siasa za upinzani Tanzania?

Pia wadadisi tulihoji kwa nini ilikuwa ngumu kuachia jimbo analotaka kugombea Makamu Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, Tanzania bara?

Na kwa nini NCCR ilipewa majimbo tasa, kama Ilala? Aidha, kama ni kweli moja ya kigezo cha chama kuachiwa jimbo ilikuwa ni matokeo ya 2010 ya chama kilichokuwa cha pili, ni kwa nini Chadema iling'ang'ania Jimbo la Buyungu ambalo NCCR-Mageuzi ilikuwa ya pili?

Pia kwa jimbo la Mafia, CUF ilipata kura zaidi ya 6,000 kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 na Chadema ikaambulia kura 200 pekee. Sasa waliling'ang'ania kwa vigezo gani kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015?

Vigezo hivi vinatumika dhidi ya vyama vingine lakini lilipokuja jimbo lenye maslahi ya viongozi wa Chadema, vigezo havikuzingatiwa na badala yake vikachakachuliwa. Hii ilikuwa ni undumilakuwili wa wazi na ulaghai wa kisiasa. Na haya majimbo niliyotaja ni mfano mdogo, yalikuwepo mengi.

Naamini Makonda ni mzoefu sasa wa hizi siasa za wapinzani, asiwasubiri wapande majukwaani ili awajibu aanze sasa kusafisha njia kwa ajili ya CVM.

Hawa jamaa wa upinzani hawawezi kuwa na jipya katika kipindi hiki zaidi ya kuja kuibuka kwenye chaguzi ziijazo hususani ule wa mwaka 2025 na baada ya hapo watapotea tena hadi mwaka 2030!

Asiwaamshe, acha walale usingizi wa pono kama kawaida yao!

Wakistuka wakute watu wanaimba 'CCM hyena hyena, CCM nambari wani' hapo mwaka 2025!

*Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya; 0768 888 787.*

Afya

# Hatari ya simu kuiacha ikiichaji usiku kucha

Kuiacha simu yako kwenye chaji usiku kucha si jambo la lazima

Wakili mmoja (jina limehifadhiwa), alikuwepo katika mahakama ya Islamabad akifuatilia kesi yake aliyokuwa akiisimamia.

Akiwa amevalia nadhifu suti yake, ghafla moshi ulianza kufuka ndani ya koti lake jeusi na kutoka nje.

Baada ya Wakili huyo kuiona hatari hiyo, haraka haraka alilivua koti lake na kulitupa chini, lakini simu yake iliyokuwa ndani yake, ilikuwa tayari imekwisha kuteketea kwa moto.

Katika video iliyorekodiwa nje ya mahakama, wakili huyo alielezea sababu ya kulipuka kwa betri ya simu yake kuwa ni kutokana na kuiweka chaji usiku kucha.

''Niliiweka simu yangu kwenye chaji usiku kabla ya kulala na kisha kuiondoa asubuhi, labda ndiyo sababu ya kuliepuka,'' anasema Wakili huyo.

Kumekuwa na matukio ya milipuko ya betri kwa baadhi ya simu hasa siku za nyuma.

Mapema mwaka 2020, akizungumza na gazeti la The Daily Mail, mkazi wa California nchini Marekani, alidai betri ya simu yake ililipuka ghafla na kusababisha simu yake ya mkononi kuteketea kabisa.

Baada ya video ya kulipuka kwa simu ya yule Wakili wa Islamabad kusambaa, Watumiaji wengi wa simu wanauliza je, ni hatari kuacha simu katika chaji usiku kucha?

Wataalam wanashauri kwamba ni vema kuchaji simu kati ya asilimia 20 na 80 kwa wakati mmoja.

Kwa mujibu wa jarida la sayansi na teknolojia la 'The Conversation,' simu nyingi za sasa hujaa chaji chini ya dakika 30.

Muda unaohitajika kuchaji pia unategemea na uwezo wa betri ya simu na ni kiasi gani cha nishati inayotolewa na chaja yako.

Kuiacha simu kwenye chaji usiku kucha, si jambo la lazima na pia husababisha uwezo wa betri ya simu yako kupungua kwa kasi, hivyo hudhoofisha betri ya simu.

Wataalamu wanashauri kuepuka kuchaji simu kutoka sifuri hadi asilimia 100 (yaani kuchaji betri ya simu hadi asilimia 100 kwa mara moja).

Mathalani, mwongozo wa simu za Samsung, unasema kuchaji simu hadi asilimia 100, mara nyingi kunaweza kudhuru afya ya betri ya simu yako.

Kwa mujibu wa wataalamu, ni bora kuchaji simu kati ya asilimia 20 na 80 kwa wakati mmoja.

Hata hivyo, wataalamu wanasema kuna uwezekano mdogo wa simu kulipuka kwa kuichaji muda mrefu. Bali hulipuka kutokana na kasoro nyingine katika betri.

Kwa kawaida, waya wenye hitilafu wakati wa kuchaji au betri kutoweza kumudu joto, kunaweza kusababisha kulipuka.

Profesa Clare Gray, mtaalamu wa nishati katika Chuo Kikuu cha Cambridge nchini Uingereza, aliambia BBC kuwa makosa madogo yanaweza kusababisha betri kulipuka, kama vile chuma kilichoachwa kwa bahati mbaya kwenye betri.



**TAHADHARI ZA KUCHUKUA**

Wataalamu wanashauri kuepuka kuchaji simu kutoka sifuri hadi asilimia 100

Baadhi ya hatua zinaweza kuifanya betri ya simu yako kufanya kazi kwa muda mrefu na pia inaweza kusaidia kukulinda kutokana na ajali inayoweza kutokea.

Hakikisha programu za simu yako hazijapitwa na wakati.

Tumia chaja ya asili au zilizoidhinishwa za simu kwani chaja nyingine zinaweza kuwa na namna tofauti ya kupeleka moto.

Weka simu mbali na joto kali na baridi kali sana. Digrii sifuri hadi digrii 35, ni hali joto inayofaa.

Usiache simu yako ikichaji usiku kucha na ikiwa betri imejaa iondoe kwenye chaji mara moja. Fuatilia betri yako ili kuona kama inaisha chaji haraka.

Iwapo unahisi simu yako inapata joto au betri imevimba, ipeleke kwenye duka lenye betri za kampuni ya simu yako kwa ajili ya kununua betri mpya.



# Faida kiafya za kutembea kinyumenyume



**Na Mwandishi Wetu kwa msaada wa Mitandao**

MIONGONI mwa mazoezi mepesi na yasiyo na masharti makubwa, ni yale ya kutembea. Kutembea ni njia rahisi za kufanya mazoezi.

Kutembea kwa kurudi nyuma, huenda ikawa si mazoea ya kawaida, lakini kunatajwa kuleta uimara kiafya hata usawa kimwili.

Kutembea hakuhitaji vifaa maalum au uanachama wa sehemu za mazoezi, yaani (gym); na bora zaidi ni bure kabisa kwa sababu unaweza kufanya hivyo bila malipo kwa sababu una uamuzi juu ya miguu na mwili wako kwa jumla.

Ukweli ni kwamba wengi wetu kutembea ni kitu tunachofanya kama ni jambo la kawaida tu.

Haihitaji juhudi za makusudi, kwa hivyo, wengi wetu hatukumbuki faida iliyopo kwa afya zetu.

Lakini huenda ukajiuliza nini kitatokea ikiwa tutaacha kutembea kawaida tu na kuanza kutoa changamoto kwa akili na miili yetu kwa kutembea kurudi nyuma?

Sio tu mabadiliko ya mwelekeo ambayo yatatokea na kuhitaji umakini zaidi, inaweza pia kuleta faida zaidi za kiafya.

Muhimu kutambua kuwa shughuli za kimwili si lazima ziwe ngumu.

Iwe ni kawaida kwa wewe kutembea kila siku au la, kutembea kila siku kunaweza kukupa manufaa mengi ya kiafya na yanaweza kuhesabiwa kulingana na mapendekezo ya Shirika la Afya Ulimwenguni ili kupata angalau dakika 150 za shughuli za mazoezi ya viungo kwa wiki kama wanavyosema.

Hata hivyo, kutembea ni jambo gumu zaidi kuliko wengi wetu tunavyofikiri.

Kusimama wima kunahitaji uratibu kati ya mifumo yetu ya kuona, vestibular kwa Kiingereza (hisia zinazohusiana na harakati kama vile kugeuka, au kusonga haraka), na mifumo ya kustahimili (ufahamu wa mahali ambapo miili yetu iko angani).

Tunapotembea kwenda nyuma, akili zetu huchukua muda mrefu kushughulikia mahitaji ya ziada ya kuratibu mifumo hii kwa sababu inatumia akili nyingi kufikiria kupiga hatua kwa sababu si mazoea.

Hata hivyo, kiwango hiki cha juu cha changamoto huleta faida kubwa za kiafya.

Mojawapo ya faida za kutembea kwenda nyuma ni uthabiti na usawaziko ulioboreshwa.

Kufanya mazoezi kunaweza kutusaidia kuboresha mwendo wetu wa kawaida (yaani kwenda mbele) na katika suala la kuboresha usawa, husaidia watu wazima wenye afya nzuri na wale walio na ulemavu wa yabisi kavu inayozorotesha mifupa ya maungo yaani osteoarthritis ya goti.

Wakati wa kutembea kwenda nyuma tunachukua hatua fupi na za haraka, ambayo inaboresha uvumilivu wa misuli ya chini ya mguu na kupunguza mzigo kwenye viungo.

Mbinu hii imetumika hata kutambua na kutibu usawa na kasi ya kutembea kwa wagonjwa wenye matatizo ya neva au baada ya kuugua kiharusi cha muda mrefu.

Kuongeza kasi na kutembea juu au chini kwenye mteremko kunaweza pia kubadilisha aina mbalimbali za mwendo wa viungo na misuli yako, na kupunguza maumivu kwa hali kama vile plantar fasciitis, yaani, ugonjwa wa misuli mojawapo ya sababu za kawaida za maumivu ya kisigino.

Mabadiliko ya mkao yanayosababishwa na kutembea kwenda nyuma husababisha matumizi zaidi ya misuli inayounga uti wa mgongo.

Hii inaonyesha kwamba kutembea kwenda nyuma kunaweza kuwa zoezi la manufaa kwa watu wenye maumivu ya muda mrefu ya sehemu ya chini ya mgongo.

Mbinu hii imetumika hata kutambua na kutibu usawa na kasi ya kutembea kwa wagonjwa wenye matatizo ya neva au baada ya kupata kiharusi cha muda mrefu.

## MABADILIKO KATIKA NGUVU TUNAYOTUMIA:

Manufaa ya kubadilisha maelekezo si ya matibabu pekee. Kuvutiwa na kutembea kurudi nyuma kumesababisha watafiti kugundua manufaa mengine.

Ingawa kutembea kawaida kunaweza kutusaidia kudumisha uzani mzuri, kutembea kurudi nyuma kunaweza kuwa na ufanisi zaidi.

Gharama ya nishati na mabadiliko haya ni karibu asilimia 40 zaidi kuliko kutembea kwa kasi sawa mbele: 6.0 Mets dhidi ya 4.3 Mets (moja ya metabolic sawa, Met, ni kiasi cha oksijeni inayotumiwa wakati wa kukaa kupumzika).

Utafiti mmoja ulionyesha kupunguzwa kwa mafuta ya mwili kwa wanawake waliomaliza mafunzo ya kukimbia kwa wiki sita au kufanya mazoezi ya kutembea kwa kurudi nyuma.

Tunapojiamini kwa kutembea kurudi nyuma, kusonga mbele na kukimbia kwa namna hii kunaweza kuongeza mahitaji hata zaidi.

Ingawa mara nyingi husomwa kama zana ya urekebishaji, kukimbia kurudi nyuma huongeza uimara wa misuli ambayo ni muhimu kwa kunyoosha goti, ambayo si tu hutafsiri kwa kuzuia majeraha, lakini pia kwa uwezo wetu wa kutoa nguvu na utendaji.

Kukimbia kurudi nyuma kwa kasi hupunguza nishati tunayotumia tunaposonga mbele.

Maboresho haya yana manufaa hata kwa wakimbiaji wenye uzoefu ambao tayari wana mbinu ya kukimbia kwa ufanisi zaidi.

Ikiwa kutembea kurudi nyuma inakuwa rahisi sana na mapungufu ya nafasi yanaonekana kufanya mazoezi ya kukimbia huku, njia nyingine ya kuongeza ugumu ni kuanza kuburuta uzani.

Kuongeza mzigo wa jumla huongeza matumizi ya misuli ya goti inayopanuka huku ukiweka mahitaji mazito kwenye moyo na mapafu kwa muda mfupi.

Kutembea kinyumenyume na uzani kunaweza kuboresha nyakati za kawaida za kukimbia kwa wanariadha wachanga.

Kutembea kwa kigari cha kuteleza na kukirudisha nyuma kuna hatari ndogo ya kuumia, kwani matokeo yanayowezekana ikiwa tumechoka kupita kiasi ni kwamba hakitasonga.

Lakini kwa uzani mwepesi, aina hii ya mazoezi inaweza kutoa kiwango cha kutosha cha upinzani ili kuchochea uboreshaji mkubwa katika nguvu za mwisho zile kidogo.

Kwa uzani wa kuburuta chini kama asilimia 10 ya uzito wa jumla wa nyakati bora za kukimbia zinaweza kupatikana kati ya wanariadha wachanga.

## JINSI YA KUANZA KUFANYA MAZOEZI HAYO:

Kutembea kurudi nyuma sio ngumu, lakini hiyo haimaanishi kuwa ni rahisi.

Kwa hivyo, unaongezaje hii kwa utaratibu wako wa mazoezi?

Tunaporudi kinyume nyume kuna uwezekano mkubwa wa kukosa vizuizi na hatari ambazo tunaweza kugonga au kuanguka, kwa hivyo, kwa ajili ya usalama ni bora kuanza ndani ya nyumba, ambapo unajua hutagongana na kitu au mtu au ufanye mazoezi hayo katika sehemu iliyo wazi na tambarare.

## ZUIA JARIBU LA KUGEUZA MWILI WAKO NA KUTAZAMA JUU YA BEGA LAKO:

Weka kichwa chako na kifua chako juu unaponyoosha kidole chako kikubwa nyuma kwa kila hatua, ukisonga mguu wako kutoka kwenye vidole hadi kisigino.

Mara tu unapokuwa na ujasiri zaidi, unaweza kuharakisha, kuhakikisha kuwa unatumia reli za mwongozo inapohitajika.

## IKIWA UNATUMIA UZITO, ANZA NA UZITO WA CHINI:

Zingatia seti nyingi badala ya umbali mrefu, na kumbuka kudumisha uadilifu wa mbinu yako kwa umbali usiozidi mita 20 wakati unaanza.

Kurunzi

# Taasisi hizi zina dhima kubwa kusimamia malezi ya watoto



**Na Dk. Reubeni Lumbagala.**

HIVI karibuni, niliandika makala iliyokuwa na kichwa: "Familia isijitenge na malezi sahihi ya watoto." Nilijielekeza kwenye taasisi ya familia kwa kuwa ni taasisi ya kwanza kabisa katika malezi na maadili bora ya watoto.

Nilieleza kadri nilivyoweza namna wazazi na wanafamilia kwa ujumla walivyo na wajibu mkubwa wa kumtengeneza mtoto kabla taasisi nyingine hazijaonesha mchango wao wa kimalezi.

Malezi na maadili ya watoto ni jambo linalohitaji ushirikiano wa taasisi mbalimbali ili mtoto akue katika maadili, nidhamu na hatimaye kuwa raia mwema kwa Taifa lake.

Katika makala haya nitajaribu kadri nitakavyojaaliwa kuonesha jinsi taasisi nyingine tofauti na familia zilivyo na nafasi kubwa ya kujenga maadili na malezi bora kwa watoto.

Moja, taasisi za kiroho. Hizi ni taasisi za kidini. Dini zote kupitia mafundisho yake zinafundisha mtoto na watu wote kwa ujumla kuwa na maadili mazuri. Mafundisho ya dini yanakazia sana suala la tabia njema, kuwaheshimu wakubwa na wengine, nidhamu, kuwa na hofu ya Mungu na kuchukia uovu.

Mtoto au kijana aliyelelewa katika mafundisho ya kiroho atawapendeza wengi kuanzia Mwenyezi Mungu aliyetuumba, wazazi, ndugu, majirani, walimu na viongozi.

Hata matatizo ya kijamii yaliyopo nchini kwetu na duniani kama uhalifu, rushwa, dawa za kulevya, ukahaba na wizi, ni miongoni mwa mwa matokeo ya kutozingatia mafundisho ya kiroho kutoka kwa viongozi wetu wa dini.

Watoto na vijana wanapaswa kupewa maadili na malezi bora ili kuepuka kujiingiza katika kufanya maovu hayo.

Nakumbuka Mwigulu Nchemba akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, wakati wa maadhimisho ya miaka 57 ya Ushirika wa Wanafunzi wa Kiinjili wa Tanzania (Tafes) yaliyokwenda sambamba na kusherehekea miaka 27 ya uwepo wao hapa nchini, alisema maandalizi ya maadili mema yanaanzia katika ngazi ya familia na taasisi za kiroho. Aliongeza kusema kwamba uhalifu wa kikatili ni zao la kutokuwepo kwa hofu ya Mungu kwenye mioyo ya watekelezaji wa matukio ya aina hiyo.

"Tukiwa na watu waliolelewa katika misingi ya imani, hatutaweza tukapata watu wasiojulikana (Wahalifu) na jambo hili linaniudhi sana. Hatuwezi tukawa na watu wasiojulikana wanaotenda uhalifu na kukimbia kusikojulikana na tutashughulika nao kupitia nguvu za dola".

Ni kweli kuwa kama watoto na vijana watazingatia mafundisho ya dini vizuri basi tutaisaidia sana hata serikali yetu katika kupambana na maovu katika kijamii ambayo husababishwa na kutozingatia mafundisho ya maadili ya dini.

Mbili, taasisi za elimu.Walimu pamoja na kuwa na jukumu kubwa la kuwafundisha watoto masomo ya darasani lakini pia wanawajibika kuwalea watoto katika malezi na maadili mema.

Ndio maana mwalimu yeyote ni lazima asomee somo la saikolojia na hongozi anapokuwa chuoni. Kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, watoto na vijana hufundishwa maadili na tabia njema na walimu wao.

> **Tukiwa na watu waliolelewa katika misingi ya imani, hatutaweza tukapata watu wasiojulikana (Wahalifu) na jambo hili linaniudhi sana. Hatuwezi tukawa na watu wasiojulikana wanaotenda uhalifu na kukimbia kusikojulikana na tutashughulika nao kupitia nguvu za dola**

Kupitia mada zinazofundishwa katika masomo yao, watoto na vijana hujifunza mambo mengi mazuri ambayo kama watazingatia yatawasaidia katika maisha yao ya sasa naya baadae. Hufundishwa nidhamu, utii wa sheria, kufanya kazi, kuishi kwa ushirikiano, kuepuka tabia mbaya, kuwasaidia wengine, usafi, nk. Mtoto anayezingatia haya anajijengea kesho yake nzuri sana katika maisha yake.

Katika shule za msingi na sekondari, wapo walimu wa madarasa, walimu walezi wa wanafunzi wa kiume (patrons) na walimu walezi wa wanafunzi wa kike (matrons), hawa wote wamewekwa kuwa karibu sana na wanafunzi katika kuwalea wanafunzi katika malezi bora.

Katika vyuo vikuu wapo washauri wa wanafunzi (Dean of Students) ambao wamewekwa ili kuwasaidia wanafunzi kutatua changamoto zao pale wanapohitaji msaada na pia kuwasaidia vijana wa vyuo vikuu kuwa na maadili na tabia njema.

Walimu hawa kwa kushirikiana na walimu wenzao wanashirikianna katika kupanda mbegu nzuri ya maadili na malezi kwa watoto na vijana.

Tatu, serikali. Serikali ina wajibu mkubwa wa kutunga sheria, sera na kuzisimamia ipasavyo ili kuwasaidia watoto na vijana kukua katika maadili na malezi bora.

Serikali kupitia sheria inawawajibisha wazazi wote wanaoshindwa kuwatunza watoto wao ambao hupelekea watoto na vijana kujiingiza katika vitendo viovu kama ukahaba na wizi.

Sheria zinazotungwa ni muhimu zilenge kuwalinda watoto dhidi ya ukatili, ndoa za utotoni, manyanyaso na vitendo viovu kama ubakaji vinavyofanywa na wasiopenda au kutojali maendeleo ya watoto na vijana. Naamini serikali ikifanya hivyo, watoto na vijana watakuwa katika malezi bora ambayo ni chachu ya maendeleo ya Taifa lolote.

Kama kundi la watoto na vijana litapuuzwa na kutelekezwa, basi kama Taifa tutakuwa na kazi kubwa ya kujenga upya nchi yetu katika malezi na maadili.

Miongozi mwa maeneo muhimu ya uwekezaji katika nchi yetu ni katika watoto na vijana. Kwa hiyo familia, taasisi za dini, taasisi za elimu kwa kushirikiana na serikali huchangia malezi bora ya watoto na vijana. Ni muhimu kwa taasisi hizi kushirikiana kikamilifu kwenye malezi na maadili ya watoto.

*Dk. Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni (+255) 620 800 462.*



Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Watu wanaoanza kujitambua hawafanyi haya



KUJITAMBUA si tu kuwa mwerevu, bali pia ni kufanya maamuzi sahihi na kuepuka tabia zitakazokusambaratisha. Kuna vitu ambavyo watu wanaoanza kujitambua na wanaojitambua hawafanyi.

Nia ya makala hii ni kukusaidia ili kuhakikisha na wewe kama unajitambua na kama unapanga kukua kwenye maisha yako, kuacha kufanya mambo haya au kujitenfa mbalina tabia hizi: -

**1. WANAOJITAMBUA HAWAACHI KUJIFUNZA**

ALBERT Einstein alisema maneno haya, "Maisha ni kama kuendesha baiskeli. Ili kudumisha urari wako kwenye baiskeli (balance), lazima uendelee kuendesha, ukisimama unakosa balance na kuanguka."

Watu wanaojitambua wanajifunza kila siku. Kujifunza kunawaletea busara, hekima na maarifa kwenye maeneo mbalimbali ya maisha.

Watu hawa huwa na akili inayopokea mambo mapya, wanakumbushwa mambo, wanasikiliza aina mpya ya vitu vinavyowajenga, wanafikiria, wanauliza maswali, wanasoma vitavu na majarida, wanasikiliza maoni, wanawasikiliza wanaokosoa.

Watu hawa hata wakisikiliza muziki wanasikiliza maneno fulani ya kuwajenga au kuwapa hamasa. Kwao muda ni mdogo, hivyo wanaweka muda kujiboresha kuliko kuzungumzia uvumi na porojo.

Kwa hiyo, ukichunguza kidogo utagundua kwamba jamii yetu ina shida kidogo linapokuja suala la kujisomea, kusikiliza redio au hata kutazama runinga ili kujipatia maarifa mapya.

Watanzania wengi wamekuwa wavivu sana wa kusoma hasa mambo yanayohusu maarifa. Usomaji wa magazeti ambayo yana kawaida ya kuandika mambo kwa kina na mtu anakuwa na uwezo wa kufanya rejea yanapungukiwa wasomaji kila uchwapo.

Watu wanapenda vitu vidogovidogo na upuuzi na ndio maana wako sana kwenye mitandao ya kijamii lakini si ile inayolenga kutoa maarifa.

Ukiona mtu yuko 'bize' na simu yake kubwa, basi anasoma au kusikiliza umbea.

Hata majumbani mwetu watu wanakalia kutazama zaidi michezo ya kuigiza na filamu kwenye runinga au kusikiliza redio kuliko vipindi vya maarifa kama ukulima wa kisasa, mapishi na kadhalika.

Sisemi kwamba filamu na michezo ya kuigiza haina mafunzo lakini familia zinapaswa pia kujengwa vyema ili kusikiliza na kufuatilia vipindi vya maarifa.

Wazazi pia wanapaswa kuwajengea pia watoto wao moyo wa kupenda kuudadisi na kusoma vitabu.

Lakini wewe mtu mzima mwenzangu, anza sasa kujitenga na umbea, kufuatilia au kusoma vitu vyepesi na visivyo na tija na badala yake anza kutumia muda wako kwa vitu vyenye kujenga. Hakikasha kila siku unajufunza kitu kipya.

**2. WANAOJITAMBUA HAWAKUBALIANI NA MAMBO TU KIREJAREJA**

Confucius alipata kusema, "Anayeuliza swali ni mpumbavu kwa dakika; asiyeuliza ni mpumbavu maisha yote" -

Watu wanaojitambua hawaogopi kuuliza au kutilia shaka mambo. Unapohoji, inaonyesha unataka kuelewa, unataka ufafanuzi, kuchimba zaidi, unataka mawazo mapya, na inaonesha unafikiri kwa uchambuzi. Watu wa kawaida huridhika kuona mambo yapo jinsi yalivyo lakini wanaojitambua hutaka kujua kwa nini yapo kama yalivyo. Wanachimbachimba kujua undani.

**3. HAIWAINGII KWENYE MAGOMVI AU MABISHANO**

Watu wanaojitambua wanajiepusha kila inavyowezekana kubishana na watu.

Kubishana tena wakati mwingine kwa mambo hayamwongezei mtu tija kama ubishi wapira ni kujipotezea muda.

Watu wa aina hii wanajua kuwa hata ukionekana umeshinda mjadala, hupati alama za kijamii kwa hilo. Hili mara nyingi huwafanya waonekane vibaya kwenye macho ya wengine. Wanaojitambua hupenda kujadili mawazo hata na watu ambao hawakubaliani nao. Wanajua kuwa mazungumzo ya utulivu ambapo pande zote zinasikilizana kwa dhati, huleta matokeo bora kuliko majibizano makali kama yake ya ushabiki wa timu.

Ikiwa mtu fulani ana hasira wakati wa mazungumzo, watu wanaojitambua husikiliza na kujibu kwa utulivu. Ikiwa mwenye hasira ataendelea kufoka, anayejitambua ataondoka kwenye mazungumzo sababu anajua ni upotezaji wa muda na huenda kukatoke shari ambayo angeweza kuipusha au kuiepuka.

**4. WANAOJITAMBUA HAWAZUNGUMZI BILA KUFIKIRI KWANZA**

Anthony Liccione alisema, "Mjinga anakuwa mjinga zaidi pale ambapo mdomo wake unakuwa wazi kuliko akili yake."

Naye Abraham Lincoln alisema, "Bora kukaa kimya watu wakadhani ni mpumbavu kuliko kusema na kuwathibitishia kuwa wewe ni mpumbavu."

Hii haimaanishi kwamba wanaojitambua kwenye jamii wanapaswa kuwa bubu. Hawakwepi kushirikisha maoni yao bali wanachukua sekunde za ziada kufikiria kile wanachotaka kusema, na wanahakikisha kile wanachosema kinaongeza thamani siyo alimradi waseme bila kupima wanachotaka kusema. Kwa kusema kidogo, unakuwa na athari kubwa katika kile wanachosema sababu watu wanakusikiliza zaidi unapozungumza.

Mwisho fikiria mtu ambaye unamjua kuwa anaongea sana, je unampa uzito? Acha kuzungumza sana, usiongee mara nyingi hata kama watu wanapenda kukusikiliza. Waache na hamu yao ili wakuhitaji kesho.

**5. WANAOJITAMBUA HAWAKARIBISHI MTAZAMO HASI**

William James alivumbua kwamba, "Binadamu anaweza kubadilisha maisha yake kwa kubadilisha mtazamo wake"

Watu wanaojitambua, wanawekeza kwanza kwenye mtazamo wao. Wanahakikisha wanawaza kujiona vizuri. Wakiitazama hatma yao, wanaitazama kwa matumaini na kwa mtazamo chanya. Wanaona mbele Kuna kufanikiwa, kushinda, wanaona uwezekano, wanaona hatua zaidi, kufaulu, wanajiona miongoni mwa watu waliofanikiwa nk.

Pamoja na mtazamo chanya, wanaojitambua hawaachi kutafiti mazingira yanayoweza kuwaletea kushindwa (Thinking in worst-case scenarios) na kuandaa mpango wa kukabiliana na mazingira haya. Mfano kama mtu ana tukio kubwa kama harusi, ni muhimu kutambua kuwa, inawezekana kuna mazingira yakaenda kombo. Mfano, je ikitokea umeme umekatika ukumbini tutafanyaje? Hii itakupelekea kuandaa jenereta.

Kuwaza mazingira yanayoweza kuharibu tukio si mawazo hasi ila ni ishara ya kujitambua zaidi. Jambo kubwa la kuzingatia ni kwamba kuanzia sasa acha kuwaza mawazo hasi, kujiona duni na mtu asiyeweza, acha kujiona hufai, kujiona wewe si bora kama wengine. Kumbuka kuwa, huwezi kufanikiwa zaidi ya unavyojiona. Kwa maana, "Ajionavyo mtu nafsini mwake, ndivyo alivyo."

Wework Consult - Your Partner in Growth.

**Itaendelea wiki ijayo…**



Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 13

**Chris anampiga mkewe akimtetea hawara yake hadi anapoteza fahamu. Baadaye analazimika kumpeleka hospitali akiwa hajitambui. Anawadanganya ndugu wa mkewe kwamba mwanamke huyo ametoweka. Daktari anamjulisha kwamba mkewe amefariki dunia, kisha anampa njia itakayosaidia asishitakiwe kwa mauaji. Chris anakubali njia hiyo lakini gharama za kuficha kifo hicho ni kubwa. Chris anayewahadaa ndugu za mkewe kwamba yuko katika harakati za kumtafuta, hatokei katika kikao muhimu cha kujulishana mahala alikofikia katika kumtafuta. Wakati ndugu wa mkewe sasa wakiwa kiguu na njia polisi, Chris anabainika kwamba kauza nyumba hali inayomsikitisha sana dada yake. Fuatana na mtunzi katika kisa hiki.**

"Wanaona kama polisi hapa Tabora wanawazingua katika kumbana bwanamdogo awasaidie kumpata mama Kenny. Jacob anasubiri mshahara uingie aende makao makuu Dodoma. Jana akizungumza na mimi kwa simu alisema asipopata ushirikiano kutoka kwa mkuu wa polisi atamtafuta hata Waziri wa Mambo ya Ndani."

"Duh! Yamekuwa hayo! Kwa hiyo wanahisi Chris kamficha?"

"Wanataka awajibike zaidi. Wanaona polisi wanamchekea kwani wanaona yeye ndiye chanzo cha yote," alisema na kuongeza kwamba anaona kama wako sahihi.

***

Ilikuwa saa tatu asubuhi, Mwalimu Misango alipofika kwenye banda la biashara la mdogo wake, Chris, lililokuwa katikati ya Mji wa Tabora.

Kwanza alishituka kwa jinsi lilivyokuwa tofauti na alivyolizoea kutokana bidhaa kupungua sana.

Bidhaa kubwa iliyokuwa ikiuzwa katika banda hilo kubwa ni mbao. Lakini pia mdogo wake alikuwa akiuza saruji, mabati, nondo, misumari, kokoto na vifaa vingine kadha wa kadha vya ujenzi.

Asubuhi hiyo, hakukuwa na bidhaa nyingine kwenye banda hilo zaidi ya mbao chache za aina mbalimbali kama muninga, mkongo na cypress. Mtu yeyote aliyelizoea banda hilo angeweza kudhani amepotea njia!

Hata pale nje hakukuwa na pilikapilika alizozoea kuziona za watu hususani makuli waliokuwa wakisubiri kuwabebea wateja mbao, baadhi wakiwa na mikokoteni na wengine pikipiki za miguu mitatu.

Aliona mkokoteni mmoja na mhusika akiwa amelala usingizi kuonesha kwamba kwa muda mrefu hakukuwa na kitu cha kumshughulisha.

"Habari za hapa binti," alimsalimia binti aliyekuwa akiuza banda hilo, Diana Masemele.

"Nzuri Mwalimu, shikamoo."

"Marahaba. Habari za hapa."

"Nzuri."

"Nzuri wakati ninaona kama banda linafilisika?"

"Mwalimu, kwa kweli hali ni mbaya. Kama nilivyokueleza siku ile Mwalimu, shida ni huyo mwanamke wake aliyempata sasa."

"Kwani anakuwa shida hadi huku kwenye biashara?"

"Yaani yeye akija hapa au ukiona simu yake basi ujue anataka hela tu."

"Kwa maelekezo ya Baba Kenny au hata peke yake tu."

"Bosi (Chris) alishasema akitaka pesa nimpe. Mara nyingi huwa anapiga simu. Yaani ukipokea tu simu yake, hata bila salamu utasikia, nitumie elfu hamsini, nitumie laki... Biashara inakufa mwalimu."

"Wewe kwa nini usikatae kisha ukae kitako na bosi wako umweleze mnaua biashara. Hii biashara ikifa hujui na wewe utakuwa huna ajira?"

"Mwalimu, niliwahi kumwambia bosi akaniambia hayo hayanihusu. Lakini ninashangaa, kamfungulia huyo mwanamke duka hivi la vipodozi lakini bado anaomba tu pesa huku."

"Duka?"

"Ndiyo. Duka la vipodozi liko karibu na Chuo cha Uhazili."

Mama Kessy aliinamisha kichwa chini akiwaza kwa muda huku akihisi moyo ukimwenda mbio kisha akamgeukia Diana.

"Hii si bure. Huyu binti atakuwa mchawi. Amemroga mdogo wangu. Si bure kabisa."

"Kama limbwata lipo, basi unaweza kusema bosi kalishwa limbwata kweli... Kaa naye Mwalimu. Biashara inakufa. Wateja wetu wamehama kabisa kwa sababu bidhaa nyingi hatuna."

Mwalimu Misango alitoa simu yake ya mkononi na kumpigia mdogo wake. Iliita mara tatu bila kupokelewa.

***

Ilikuwa siku nyingine, Mwalimu Misango alikuwa akimbembeleza Huba ambaye usiku mzima alikuwa akiweweseka na kila anaposhtuka anamtaja mama yake.

Hali hiyo ilimfanya Mwalimu kuhamia chumba kwa watoto na kulala akiwa amekumbatia mtoto huyo ambaye sasa ilikuwa ni zaidi ya miezi saba bila kumwona mama yake.

Ajabu hata Jacob alikuwa amekata mguu kuja kuwajulia hali wapwa zake na kuulizia au kujadili mustakabali wa Mama Kenny.

Wakati akijiandaa kuondoka kwenda kazini asubuhi hiyo, Huba alikuwa akilia akimtaka mama yake na kama kawaida Mwalimu akawa anampa maneno ya kumtuliza kwamba atamwona mama yake mchana huo.

> **Ni kweli, wanawe wako hapa lakini hao waliowaambia habari zake walipaswa pia kuwaambia kwamba ametelekeza watoto na hana habari nao... Kwani kafanya nini hasa mdogo wangu**

Lakini kitendo cha mtoto huyo kuweweseka sana usiku huo muda mrefu huku akimtaja mama yake kilimfikirisha sana mwalimu huyo. Kilimfanya awaze mengi kuhusu mustakabali wa wifi yake.

Haiwezekani hadi muda huo huyo mwanamke akawa kajificha mahala kwa ajili yoyote ile, hususani ya kumkomoa mumewe kama alivyowahi kumtajia. Kwa nini asikumbuke watoto wake? Na kwa nini Jacob alikuwa amekata mguu. Vipi baba wa Mama Kenny? Alijiuliza maswali mengi bila majibu.

Sasa, kama alivyokuwa akihisi Jacob, alipoteza matumaini kama Mama Kenny alikuwa mzima.

Mumewe aliyekuwa akimsubiri kwenye gari nje ili ampitishe shuleni kwake kisha aendelee kwenda kwenye kibarua chake pia alimpigia honi baada ya kuona anachelewa. Alipoiona hatokei akashuka kwenye gari na kumfuata ndani.

"Vipi, nikuache, utachukua bodaboda?"

"Nakuja Baba Kessy," alisema na baada ya takribani dakaki moja na sekunde kadhaa kisha akitoka nje ya chumba cha watoto. "Nilikuwa ninambembeleza alale kwa sababu usiku alikuwa anaweweseka sana. Nashukuru amelala."

"Huko kuweweseka asije akawa na homa?"

"Kila nikimgusa naona hana joto. Ngoja nitawahi kutoka kazini nimpeleke hospitali afanyiwe vipimo. Lakini huko kuweweseka kwake huku akimtaja mama yake kunanitisha kidogo."

"In fact hata mimi, mashaka yananizidi kuhusu wifi yako. Kwakweli ninapata wasiwasi na mustakabali wake... Twende tuwahi. Tutajadili usiku hili suala," alisema mumewe.

Wakati wanatoka, mlangoni wakakuta watu wawili wakibisha hodi.

"Karibu, mnasemaje?" Aliuliza Mwalimu Misango..

"Tunamuulizia Mwalimu Misango. Bila shaka ni wewe," alisema mmoja wao akinyooshea Mwalimu kidole cha shahada.

Mama Kessy na mumewe walitizamana. Kisha Mama Kessy akawaambia kwamba ni yeye.

"Niwasaidie nini?" Aliuliza mwanamke huyo.

"Tunamuuliza mdogo wako, Chris, kama yupo hapa."

Mama Kessy na mumewe walitizamana tena.

"Vipi kuna nini na nyinyi ni akina nani?" Anahoji mumewe.

"Hakuna kitu, yeye ni rafiki yetu tu, ila tuna shida naye kwa sababu nyumbani kwake tumeambiwa kaiuza na hakuna anayejua mahala anakoishi," alijibu mmoja wa wale wanaume wawili.

"Jamani tusidanganyane," alisrma Baba Kessy. "Mimi ninakufahamu wewe kama polisi. Si mseme tu shida yenu?"

Wale wanaume wawili waliangaliana, kisha mmoja wao akajibu: "Sawa. Sisi ni polisi na tunamhitaji Chriss kituoni."

"Chriss hatujamtia machoni kwa muda mrefu sasa. Wala hatujui mahali anapoishi baada ya kuuza nyumba yake," alijibu Mwalimu Misango.

"Mbona tumeambiwa watoto wake wako hapa. Inawezekanaje mkawa hamjui mahali aliko. Kwani huwa hata haji kusalimia wanawe?" Akazidi kuhoji mmoja wa wake askari, wote wakiwa wamevaa kiraia ingawa Misango hakuchelewa kugundua kwamba wote walikuwa wameficha bastola zao viunoni.

"Ni kweli, wanawe wako hapa lakini hao waliowaambia habari zake walipaswa pia kuwaambia kwamba ametelekeza watoto na hana habari nao... Kwani kafanya nini hasa mdogo wangu?" Alihoji Mwalimu Misango.

"Ana tatizo dogo tu kituoni," akajibu yule mwingine ambaye muda mwingi alikuwa kimya. Alikuwa mrefu kidogo kuliko mwenzake.

"Ndugu zangu kwa nini tusielezane ukweli tu. Mimi na nyinyi mwajiri wetu mmoja, Wizara ya Mambo ya Ndani. Mimi ni ofisa wa Uhamiaji. Tunaomba mtusaidie kutueleza kosa lake," alisema Baba Kessy.

"Sisi tumetumwa tu kumpeleka kituoni na huko ndiko atajua kosa lake," alijibu tena yule askari wa pili.

"Hilo ndilo kosa kubwa wanalofanya askari wa Tanzania. Nyinyi hakumjifunza kwamba ukienda kum-arrest mtu unatakiwa kujitambulisha kwa kutoa kitambulisho chako halafu unamweleza kosa lake?"

"Kwani nyinyi ndio watuhumiwa? Mngekuwa watuhumiwa tungewaambia kosa. Nadhani hakuna haja ya kuwaambia ninyi... Tunaomba kukagua nyumba yenu kama yumo ama la," alisema yule askari wa pili.

"Lakini si mnajua taratibu? Huwezi kukagua nyumba ya mtu bila kumshirikisha kiongozi wa mtaa... anaway, ninawaruhusu ili tusichelewashane," alisema Baba Kessy

Akaongozana nao wakawa wanaingia chumba kimoja baada ya kingine hadi vyooni. Wakajiridhisha kwamba Chris hakuwepo mahala pale. Kisha wakashukuru kwa kupewa ushirikiano, Wakaaga wakiomba msamaha kwa usumbufu, kisha wanaondoka.

Hata hivyo, waligoma kabisa kueleza Chris anatafutwa hasa kwa kosa gani ingawa Mwalimu Misango na mumewe walihisi ni sakata la kupotea kwa mkewe.

*Itaendelea*



# Wajue Wahouthi na kwanini wanashambulia meli zinazopita Bahari Nyekundu

Waasi wa Houthi, ambao wanadhibiti sehemu kubwa ya Yemen, wameonya kuwa watashambulia meli zote zinazopita Bahari Nyekundu kuelekea Israel.

Wahouthi wanaliunga mkono kundi la Hamas katika vita vilivyozuka Oktoba 7, mwaka huu baada ya shambulio ambalo wanamgambo wa Palestina walilianzisha dhidi ya Israel na kusababisha vifo vya watu 1,200 upande wa Israel.

Waasi hao, ambao tangu mwaka 2015, wamechukua udhibiti wa Yemen, nchi iliyo kwenye fukwe za Bahari Nyekundu wamerusha makombora na ndege zisizo na rubani dhidi ya meli za mizigo zinazovuka Mfereji wa Suez kuelekea Magharibi kutoka Mashariki na kinyume chake.

Mashambulizi haya yamelazimisha kampuni kubwa tano ikiwemo kampuni ya mafuta ya British Petroleum (BP) na kampuni za meli za MSC, CMA CGM, Maersk na Hapag-Lloyd, kutumia njia nyingine ndefu zaidi ili kulinda biashara, wafanyakazi wao, meli na bidhaa.

### KWANINI WAHOUTHI WANAILENGA ISRAEL?

Kufuatia kuanza kwa operesheni za kijeshi za Israel huko Gaza, waasi wa Houthi walirusha makombora na ndege zisizo na rubani kuelekea ardhi ya Israel.

Marekani inasema meli zake za kivita katika Bahari Nyekundu, zilinasa baadhi ya makombora na ndege hizo, huku makombora mengine yakizima kwenye Bahari Nyekundu au katika eneo la Misri.

Novemba, 2023, waasi wa Houthi waliiteka meli ya mizigo ambayo walisema ni ya Israel katika Bahari Nyekundu na kuipeleka katika eneo la pwani ya Yemen.

Israel ilisema meli hiyo haikuwa yake na hakuna Waisraeli miongoni mwa wafanyakazi wake, lakini ripoti ambazo hazijathibitishwa zilisema mmiliki wa meli hiyo anaweza kuwa ni Muisraeli.

Tangu Desemba 3, mwaka huu, Wahouthi wameshambulia meli kadhaa za kibiashara katika Bahari Nyekundu kwa kutumia ndege zisizo na rubani na makombora yaliyorushwa kutoka pwani ya Yemen wanayoikalia.

Meli za kivita za Marekani, Uingereza na Ufaransa, zimenasa mengi ya makombora hayo, lakini meli kadhaa zimeshambuliwa.

Kampuni ya Mediterranean Shipping, kampuni kubwa zaidi ya usafirishaji duniani, ilisema inaelekeza meli zake kutotumia Bahari Nyekundu. Kampuni ya Ufaransa CMA, kampuni ya Denmark ya Maersk, Hapag-Lloyd ya Ujerumani na kampuni ya mafuta ya BP, pia zilifanya hivyo.

Kamandi Kuu ya Jeshi la Marekani ilisema: "Mashambulizi haya yaliyoanzishwa na Houthis huko Yemen, yanawezeshwa kikamilifu na Iran."

Marekani imependekeza uwepo wa kikosi cha kimataifa cha wanamaji ili kulinda meli za kibiashara dhidi ya mashambulizi zaidi ya Houthi.

### HOUTHI NI NANI NA LENGO LAO NI LIPI?

Wahouthi ni kundi lenye silaha nchini Yemen la Waislamu wachache wa Kishia nchini humo, Zaidis.

Kundi hilo liliundwa katika miaka ya 1990 ili kupambana na kile walichokiona kuwa ufisadi wa Rais wa wakati huo, Ali Abdullah Saleh.

Jina lao ni kutoka kwa mwanzilishi wa vuguvugu hilo, Hussein al Houthi. Pia wanajiita Ansarolá au Wafuasi wa Mungu.

Baada ya uvamizi wa Iraq ulioongozwa na Marekani mwaka 2003, Wahouthi walipitisha kauli mbiu: "Mungu ni Mkuu. Kifo kwa Marekani. Kifo kwa Israel. Laana kwa Wayahudi na ushindi kwa Uislamu."

Walijitangaza kuwa ni sehemu ya mhimili wa upinzani unaoongozwa na Iran dhidi ya Israel, Marekani na Magharibi kwa ujumla, pamoja na Hamas na Hezbollah.

''Hilo linatoa sababu kwa nini Wahouthi wanashambulia meli zinazoelekea Israel katika Ghuba," anasema Hisham al Omeisy, mtaalamu wa Yemen katika Taasisi ya Amani ya Ulaya.

"Sasa wanapambana na mabeberu, wanapigana na maadui wa Uislamu," anasema. "Hilo linaendana vyema na msingi wake," aliongeza.

### JINSI HOUTHI WALIVYOYACHUKUA MAENEO YA YEMEN

Waasi wa Houthi walipata nguvu kubwa ya kisiasa nchini Yemen mwanzoni mwa 2014, walipoibuka dhidi ya mrithi wa Ali Abdullah Saleh kama Rais, Abd-Rabbu Mansour Hadi.

Baada ya kufikia makubaliano na Saléh, adui yao wa zamani, walikusudia kumrudisha madarakani.

Walichukua udhibiti wa Jimbo la Saada Kaskazini mwa Yemen na mapema mwaka 2015, waliteka mji mkuu Sanaa na kumlazimisha Hadi kukimbilia nje ya nchi.

Nani anawaunga mkono Houthi?

Waasi wa Houthi wanaungwa mkono na Hezbollah, kundi la waasi la Lebanon la Shia.

Hezbollah imewapa mafunzo makubwa ya kijeshi tangu mwaka 2014, kulingana na Kituo cha Kupambana na Ugaidi, ambayo ni taasisi ya utafiti wa kijeshi ya Marekani.

Wahouthi pia wanaichukulia Iran kama mshirika, kwa sababu Saudi Arabia ni adui wao wote. Iran inashukiwa kusambaza silaha kwa waasi wa Houthi.

Marekani na Saudi Arabia zinasema Iran ilitoa makombora ya balistiki ambayo Wahouthi waliyarusha katika mji mkuu wa Saudia, Riyadh, mwaka 2017, lakini yaliangushwa.

Saudi Arabia pia ililaumu Iran kwa kusambaza makombora na ndege zisizo na rubani ambazo Wahouthi walizitumia kushambulia vituo vya mafuta vya Saudia mwaka 2019.

Waasi wa Houthi wamerusha maelfu ya makombora ya masafa mafupi dhidi ya Saudi Arabia na pia wameshambulia maeneo ya Umoja wa Falme za Kiarabu.

Usambazaji wa silaha hizi umekiuka vikwazo vya silaha vya Umoja wa Mataifa. Iran imekana kufanya hivyo.

### JE, WAHOUTHI WANA NGUVU KIASI GANI?

Serikali rasmi ni Baraza la Uongozi wa Rais. Rais Abd-Rabbu Mansur Hadi alihamisha mamlaka yake mwezi Aprili 2022 na makao yake ni mji wa Riyadh.

Hata hivyo, idadi kubwa ya watu wa Yemen wanaishi katika maeneo yaliyo chini ya udhibiti wa Houthi na shirika hilo hukusanya ushuru katika sehemu ya kaskazini mwa nchi na pia kuchapisha fedha.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linamnukuu mtaalamu anayelifuatilia kundi hilo, Ahmed al Bahri, anasema mwaka 2010, Wahouthi walikuwa na wapiganaji kati ya 100,000 na 120,000, wanaojumuisha askari wenye silaha na wafuasi wasio na silaha.

Umoja wa Mataifa pia ulisema karibu watoto 1,500 walioandikishwa na waasi wa Houthi wa Yemen, walikufa katika mapigano mwaka 2020 na mamia zaidi walikufa mwaka uliofuata.

Waasi wa Houthi wanadhibiti sehemu kubwa ya pwani ya Bahari Nyekundu, ambako wamekuwa wakianzisha mashambulizi yao dhidi ya meli.

Al Omeisy anasema mashambulizi haya yamewasaidia katika mazungumzo yao ya sasa ya amani na Saudi Arabia.

"Kwa kuonyesha kwamba wanaweza kufunga Mlango-Bahari wa Mandeb katika Bahari Nyekundu, wanaweka shinikizo zaidi kwa Wasaudi wakati wa makubaliano,"

*BBC.*



# Ujuzi na vipaji ni fedha kubwa

**Na Mwandishi Wetu**

NIMETAFAKARI kwa kina na kugundua kwamba kuna pesa ipo ipo tu lakini hatuipati kwa sababu utarajibu wa maisha yetu ni wa kila mtu mmoja mmoja kujitengenezea mwenyewe pesa kwa ujuzi wake, kipaji chake, uwezo wake na mitandao yake. Tunakwama.

Mmoja anaweza kuwa mjuzi tu. Mwingine ana kipaji tu kwenye kutengeneza nyimbo za muziki. Mwingine ana pesa kubwa tu ambayo ni wazi inatakiwa iongezeke na mwingine kama Fidelis Tungaraza ana mitandao ya nguvu tu.

Baadhi ya hawa wakiungana, watatengeneza mapesa mpaka ikawa kufuru!

Watu wenye vipaji vikubwa wamegawanyika makundi yafuatayo. Wapo wasiojua kwamba wana vipaji mpaka waelezwe na wakielezwa huishia kufurahi basi. Wapo wasiojua wana vipaji na wakielezwa husema hawajui watumiaje vipaji vyao.

Wapo wenye vipaji na wanajua wanavyo lakini hawafikirii namna ya kuvifanya vipaji vyao viwatengenezee pesa.

Wapo wenye vipaji wajuao wanavyo au walioelezwa wanavyo kisha kuuliza wafanye nini ili vipaji vyao viwape pesa.

Katika hao sijui wafuatao wako wapi au walikuwa wapi; Issa Athuman Mgaya, Hamis Thobias Gaga, Said Mwamba, Zamoyoni Mogella, Mrisho Ngassa, Haruna Moshi, Ibra Radi Washokera, King Kinya, Robert Mwampembwa na David Kyungu.

Je walijijua na wanajijua waliko kina Jacob Steven JB, Riyama Ally, Ali Mtoto Seif, Ridhiwani A Pangamawe, Ghalib Mzinga, Ramadhan Mbwaduke, Edo Kumwembe, Saleh Ally Jembe na wengi wengine wa shughuli tofauti mimi binafsi niliowaona na ninaowaona wako vizuri. mno kwenye shughuli zao tofauti.

Hebu mtazame Pangamawe. Huyu ni mjuzi mno wa muziki.

Hupiga solo kali kwa kulibadili milio kama walivyofanya kina Diblo Dibala, Dally Kimoko na Nene Tchakou.

Msikilize kwenye ule wimbo wa mwaka 1991 wa Ushinde Moyo. Msikilize kwenye Arabia, Penzi Kizungumkuti, Tulikotoka ni Mbali, Mwana Mkiwa, Asina na Mwana Makutubi miongoni mwa nyimbo nyingi za Msondo alizokamata mpini.

Jambo la kusisimua, kwenye album ya Queen Kase ya mwaka 1989, Panganawe ndiye alipiga solo kwenye nyimbo karibu zote ukiwemo huo Queen Kase wenyewe. Nilimuona akipiga solo na kinanda kwenye wimbo Ole Bado Wasumbuka kama afanyavyo siku hizi kwenye wimbo Sogea Karibu wa mwaka 1979.

Je Pangamawe anajua kuwa ana kipaji kikubwa? Je anahitaji atengeneze pesa kwa kipaji hicho? Peke yake hawezi.

Anatakiwa aungane na wajuzi wenzake wa kuimba kwa sauti za kusikika kwa tofauti, nzito na laini wakiimba sauti ya pili na ya kwanza.

Yeye apige solo na kinanda halafu awepo mwingine apige rythm. Vinatosha sana ukichanganya vya kugonga gonga na kutikisatikisa vya waimbaji wao.

Nyimbo? Hizi zitatengenezwa na Mtaalam wa kazi hiyo. Imetosha? Hapana. Anahitajika mwenye pesa kufanikisha mradi huo. Bado, mwenye mtandao mkubwa wa wadau mbalimbali wakubwa anahitajika kuifanya kazi hiyo ipenye sehemu nyingi duniani kwa biashara kubwa. Faida itagawiwa kwa kila mshiriki wa mradi huo. Bila kwenda kama ilivyo kwenye mfano huo, kila aliyejaaliwa chake atabakia nacho bila mafanikio yoyote makubwa.


Hata kama haupendi ukocha, kwa nini pale kwa Moro Kids usimchukue Zamoyoni Mogella na kumpa jukumu la kutengeneza chipukizi wafungaji mabao wa uhakika? Tutafakari.



Ridhiwani Pangamawe



Gaga na Kizito



Said Mwamba Kizoto



Riyama Ally



Mrisho Ngassa



Jacob Steven JB



Diblo Dibala




Dally Kimoko

# Kikosi cha Taifa Stars AFCON 2024

**MAGOLIKIPA:**

Kwesi Kawawa — KIF Sweden
Beno Kakolanya — Singida FG
Metacha Mnata — Yanga SC
Aboutwalb Mshery — Yanga SC
Aishi Manula — Simba SC







**WALINZI :**

Bakari Mwamnyeto — Yanga SC
Ibrahim Bacca — Yanga SC
Dickson Job — Yanga SC
Nickson Kibabage — Yanga SC
Haji Mnoga — Aldershot Town
Abdi Banda — Richardson Bay
Novatus Dismas — Shakhtar
Lusajo Mwaikenda — Azam FC
Mohamed Hussein — Simba SC
Israel Mwenda — Simba SC
Adam Kasa — IFK Haninge
Lameck Lawi — Coastal Union
Kennedy Juma — Simba SC
Zion Chebe Nditi — Aldershot Town
Abdulmalik Zakaria — Namungo
Roberto Yahya Nditi — Fofar
Miano Danilo — Villena
Mark John — Kingston FC
Edwin Balua — Tanzania Prisons







**VIUNGO:**

Mudathir Yahya — Yanga SC
Himild Mao — El Gaish
Adolf Bitegeko — VIF Iceland
Yusuph Kagoma — Singida FG
Baraka Majogoro — Chippa
Feisal Salum Abdallah — Azam FC
Mohamed Ali Omar — Borehem
Twariq Abdillahi — Telford
Morice Abraham –RFK Serbia
Kibu Denis — Simba SC
Mzamiru Yassin — Simba SC
Khieffin Hamdoun — Muscut Oman.
Said Hamisi — Jedinstov
Tarryn Allarakhia — Wealdstone
Sospeter Bajana — Azam FC







**WASHAMBULIAJI:**

Clement Mzize — Yanga SC
Cyprian Kachwele — Vancouver
Amahi Perregrino — Bodo/Glimt
Ayoub Bilahi — Free agent
Ladack Chasambi — Mtibwa sugar
Ben starkie — Llkeston
Abdul Sulemani Sopu — Azam FC
Mbwana Samatta — PAOK
Charles M'mombwa — Macarthur
Matheo Anthony — Mtibwa sugar
Adam Salamba — LY stade club
Simon Msuva — Free agent
Onary Mvungi — Nantes
Ibrahim Joshua — Tusker






**Muhimu**

Hii ni Orodha ya wachezaji (53) ambao wameitwa katika kikosi cha awali cha timu ya taifa. Katika majina haya wachezaji wa ndani ni (25) na wachezaji wanaocheza soka nje ya nchi ya Tanzania ni (28).





# Tuepuka lugha ya udhalili kwa wachezaji

**Na Ibrahim Mkamba**

NI kawaida sana kusikia anazungumziwa mchezaji wa soka wa Yanga au Simba wa kutoka nje anayeaminika hachezi vizuri kwa kuitwa majina ya kuudhi kama galasa, bomu, mzigo, mbovu, hafai na majina mengine ya ovyo kabisa utadhani wachezaji hao ni vitu visivyo uhai au wanyama!

Itasemwa na baadhi ya mashabiki wa Simba kuhusu wachezaji kadhaa wa kutoka nje wa Simba kwamba hapa tumepigwa, hapa watu wamepiga pesa na mengine ambayo si tu hudhalilisha wachezaji hao bali pia hudhalilisha waliohusika kuwaleta. Kauli kama hizo hazitolewi na mashabiki wa Yanga kwa mchezaji wao yeyote.

Kwa wachezaji wa nje wa Yanga udhalilishaji wao hutoka zaidi kwa baadhi ya wachambuzi wa soka na mashabiki wa Simba lakini kwa wachezaji wa nje wa Simba wasiokubalika hudhalilishwa na baadhi ya wachambuzi wa soka, mashabiki wa Yanga na mashabiki wa Simba wenyewe kama ilivyoelezwa hapo juu.

Kwa kweli si vizuri kumdhalilisha mtu kutokana na utendaji wake. Kama unauongelea udhaifu wake, utapungukiwa nini ukitumia maneno kama bado hajawa vizuri, anapitia changamoto za kiutendaji, moto wake haujawaka, bado anapambana na changamoto za kiuchezaji na kauli nyingine za heshima kama hizo?

Tunapaswa tuwaheshimu wacheza soka kwa sababu kila mtu anastahili heshima. Hivi tukijenga utamaduni wa kuita majina ya kuudhi watendaji wanaokosea wa sehemu mbali za utendaji, tutakuwa tunajenga taifa la watu gani?

Huduma ya muhimu inapokosekana, huwezi kusikia wahusika wa utoaji wa huduma hiyo wakiitwa wa ovyo, wabovu, magalasa na kadhalika bali utasikia ikisemwa utaratibu huu unaudhi, unatutesa, unakwamisha mambo yetu au taasisi hii inaudhi.

Tuweke akiba ya maneno kuhusu viwango tunavyoamini vya chini vya wachezaji wapya wa timu zetu. Si jambo la ajabu mchezaji akibadili timu kutowika mara moja kwenye timu mpya kama alivyowika alikotoka. Mkumbuke Torres wa Liverpool na wa Chelsea, Hazard wa Chelsea na wa Real Madrid, Coutinho wa Liverpool na wa Barca na wengine wengi.

Unasemaje mchezaji ni galasa au bomu wakati alikuwa mfungaji bora wa ligi moja ya moja ya nchi za kiafrika zenye soka kubwa? Anakuwaje galasa leo mchezaji aliyekuwa mfungaji bora, mwenye pasi nyingi za mwisho na mchezaji bora wa ligi moja ya Afrika?

Nyinyi wachambuzi wa soka, mlipojua wachezaji hao wanakuja kwenye timu zetu, mliwajadili kwa kuwapamba mno kwa kuzingatia rekodi zao nzuri za kule walikotoka. Leo vipi nyinyi hao hao mnawaponda wachezaji hao hao kwa sababu wameanza kwa moto wa chini hapa?

Hivi mchezaji bomu anawezaje kuwa nahodha wa timu ya taifa ya wachezaji wachezao nyumbani wa moja ya nchi za Afrika zilizo juu kisoka barani humu?

> “Unasemaje mchezaji ni galasa au bomu wakati alikuwa mfungaji bora wa ligi moja ya moja ya nchi za kiafrika zenye soka kubwa? Anakuwaje galasa leo mchezaji aliyekuwa mfungaji bora, mwenye pasi nyingi za mwisho na mchezaji bora wa ligi moja ya Afrika?

Tuwe tukitumia lugha za staha kuwaongelea wachezaji wa nje ambao bado hawajawaka kiuchezaji. Tutaumbuka. Hata Nonda Shaaban hakuanza kwa vishindo hapa lakini kule Ulaya akawa mmoja wa wachezaji wakubwa wa dunia. Dejan yuko sasa kwenye timu ya daraja la pili nchini kwao Serbia ya OFK Beograd akicheza mechi 10 na kufunga mabao matano.

Leo unamwita mchezaji galasa, kesho anakuolea dada yako. Utamtazamaje? Eti “hapa tumeliwa, watu wamepiga pesa hapa.” Ujasiri wa kusema hivyo unautoa wapi wakati wote tulimuona mchezahji huyo alivyokuwa akikiwasha sana kwenye moja ya timu za maana za Afrika?

Unatoaje kauli hiyo kwa waliomleta wakati uliuona ukali wa mchezaji huyo kabla hajaletwa na ukielezwa kuhusu ufungaji bora wake na uchezaji bora wake wa msimu kule alikotoka?

Hebu tuheshimiane jamani. Kila mtu anastahili heshima na wachezaji wa soka ni watu wanaostahili heshima kama watu wengine. Tuwaongelee kwa ‘favourable connotations’ na si ‘unfavourable connotations’ tufanyavyo.






Kona ya **Urembo**

Na Hidaya Machuppa
Simu: +255 765 828 219

# Kucha nadhifu huleta umaridadi

FIKIRIA kwa sekunde moja ulipitishwa kwenye ulimwengu unaoendeshwa na karmic wa Earl. Lakini kila aliponyoosha mkono wake, kuona aina ya kucha zake alizaa wazo chanya. Kucha zake chafu na zilizopauka hubeba dalili za uzembe na ujinga. Sio tu mbaya, pia ni mbaya.Vivyo hivyo kwa kucha za miguu. Kupuuza kuitunza inatosha kudhoofisha utu wako. Unahitaji kuzingatia kwa karibu kucha zako kama vile unavyojali uso na ngozi yako.

**Kucha safi**

Ni rahisi sana kuweka kucha safi. Tumia unawaji mikono bora kwa hili. Safisha kwa upole uchafu kwenye kucha. Usiweke shinikizo nyingi. Mara nyingi katika kazi ya kila siku, misumari na ngozi karibu nayo hupata makovu. Chovya vipande vichache vya maji ya limao kwenye maji ya uvuguvugu ili kuondoa madoa haya. Juisi ya limao pia huondoa madoa na kuongeza uzuri wa kucha zako. Sugua na maji ya sabuni na kitambaa cha pamba ili kusafisha kucha. Kucha zinapaswa kusafishwa mara mbili kwa siku ili kuhifadhi uzuri huu.

**Manicure-pedicure inapaswa kufanyika mara moja kwa wiki.Ulaini wa kucha**

Baada ya kusafisha kucha safi maji ambayo yamekusanyika kwenye kucha yenye kitambaa. Ikiwa maji hujilimbikiza kwenye kucha, inaweza kusababisha maambukizi. Sasa tumia cream nzuri ya unyevu kwenye vidole na massage kwenye misumari na ngozi ya jirani. Hii itaweka ngozi karibu na kucha zako laini. Unaweza kutumia mafuta ya mizeituni, almond au castor kwa kucha zako.

**Afya ya kucha.**

Kucha zako nzuri zinaonyesha utu wako na afya njema. Ikiwa kucha ni laini, laini na nyekundu, inamaanisha mwili wako pia una afya. Kucha ziliyovunjika, ziliyofifia na zenye rangi hubeba ishara za ugonjwa wowote au usawa wa kimwili. Kula vyakula vyenye vitamini na protini nyingi zaidi kama vile vyakula vya maziwa, matunda, matunda yaliyokaushwa na mboga za kijani huweka kucha nyororo na angavu na pia mwili.Ili kuepuka kuumia na maambukizi.









Kucha ndefu, zenye ncha kali zinaweza kujeruhiwa kwa urahisi au zinaweza kusababisha majeraha kwa wengine. Wanaweza pia kuwa na bakteria, ambayo inaweza kusababisha maambukizi. Ni muhimu kuweka kucha zako fupi ili kuzuia matatizo haya.

**Ili Kuboresha Kujithamini na Kujiamini kwako.**

Huduma nzuri kwa kucha inaweza kuwa njia nzuri ya kujifurahisha na kuboresha kujiheshimu kwako. Kuchukua muda wa kutunza kucha kunaweza kukufanya ujiamini zaidi na kuwa pamoja.

**Angalizo kwa utunzaji mzuri wa kucha.**

Kung'ata kucha.Tabia hizi zinaweza kuharibu kitanda cha msumari. Hata sehemu ndogo kando ya ukucha wako inaweza kuruhusu bakteria au kuvu kuingia na kusababisha maambukizi.

Tumia bidhaa nadhifu ya kuondoa rangi kwenye kucha. Punguza matumizi yako ya kiondoa rangi ya kucha. Unapotumia kiondoa rangi ya kucha, chagua fomula isiyo na asetoni.

Puuza matatizo. Ikiwa una tatizo la kucha ambalo linaonekana kutoisha lenyewe au linahusishwa na ishara na dalili nyingine, wasiliana na daktari wako au daktari wa ngozi kwa ajili ya tathmini.

Weka kucha kavu na safi. Hii inazuia bakteria kukua chini ya kucha zako. Kugusa mara kwa mara au kwa muda mrefu na maji kunaweza kuchangia kugawanyika kwa kucha. Vaa glavu za mpira za pamba wakati wa kuosha vyombo, kusafisha au kutumia kemikali kali.

Fanya usafi mzuri wa kucha. Tumia mkasi mkali wa manicure au clippers. Punguza kucha zako moja kwa moja, kisha zungusha ncha kwa mkunjo laini.

Tumia moisturizer. Unapotumia losheni ya mikono, paka losheni kwenye kucha na mikato pia.

Muone daktari wako kwaajili ya biotin. Utafiti fulani unapendekeza kwamba kiongeza lishe cha biotini kinaweza kusaidia kuimarisha kucha dhaifu

Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo Spoti
| Jumatano Desemba 27-Januari 02, 2024 |







# Simba bado kunafukuta

**Na Mwandishi Wetu**

HAMKANI hali si shwari katika kikosi cha timu ya Simba ambako mambo kama yanakwenda Msegemnege.

Wakati kukiwa kikao cha Kamati ya Nidhamu kuwajadili Clatous Chama na Nassor Kapama, Kocha wa makipa Dani Cadena amewasha moto mpya.

Cadena ambaye kabla ya Kuja kwa Abdelhak Benchikha ndio alikuwa Kaimu Kocha ameonyesha kuwa mambo hayako Sawa ndani ya kikosi hicho.

Kocha huyo ameandika kuwa kuna wakati anatamani kuchukua maamuzi yatakayoumiza magumu yatakayoumiza moyo wake.

"lakini wacha niwe Profession," ameandika.

Kauli hizo tata zinaonyeaha kuwepo changamoto ambazo huenda zikamlazimu kujiweka pembeni ili kulinda heshima yake.

## ...Yanga haijaicha salama Tabora United

**Na Mwandishi Wetu**

KIPIGO cha bao 1-0 kutoka kwa Yanga, hakijaicha Salama Tabora United. Mtafaruku umeibuka baina ya Kocha Goran Kapunovic na Mtendaji Mkuu, Thabit Kandoro.

Wa kwanza alikuwa Kapunpvic aliyesema haelewi mambo yanavyokwenda kwenye timu hiyo maana ameachiwa kila kitu na kwamba baada ya kipigo huenda ndio mwisho wake na angeenda kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa timu.

Kauli hiyo ikajibiwa na Kandoro aliyesema alisikitishwa na matamshi ya Kocha huyo.

"Sijapata taarifa rasmi lakini kibinadam nimesikitishwa, timu hii imekuwa na misukosuko kutoka FIFA ya kufungwa, nimezunguka nchi mbalimbali kuhakikisha Tabora inasimama ilipo.

"Amekuwa akilalamikia ratiba ya Ligi najaribu kumuelimisha lakini wapi hata mechi ya Yanga alilalamikia mechi kuchezwa Dodoma," alisema.

Kocha huyo aliwahi kukinoa kikosi cha Simba miaka iliyopata.



## Bingwa Mapinduzi Cup kulamba mil 100

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI timu kutoka Kenya na Uganda zikijitoa katika michuano ya Kombe la Mapinduzi, Bingwa wa atazawadiliwa Shilingi Milioni Mia Moja (Milioni 100).

Mshindi wa pili atazawadiwa Shilingi Milioni Themanini (Milioni 80).

Michuano hiyo inatarajiwa kuanza Desemba 28, 2023 katika Uwanja wa Amaan kwa Unguja na Gombani kwa Pemba.

Kamati ya michuano hiyo imeiongeza timu Jamus kutoka Sudan Kusini na JKU ya Unguja.

Timu za Bandari ya Kenya na URA ya Uganda sasa hazitakuwa sehemu michuano hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mapinduzi Cup, Mbarouk Othman alisema Kamati imefanya mabadiliko ya Makundi pamoja na ratiba na sasa makundi yamepangwa kama ifuatavyo:-

**Kundi 'A'**
Azam FC, Vitalo'o, Chipukizi na Mlandege

**Kundi 'B'**
Simba SC, APR, Singida FG na JKU

**Kundi 'C'**
Yanga SC, Jamhuri, KVZ na Jamus.

## Idriss Mbombo out, Lusajo in

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA Idriss Mbombo anatarajiwa kujiunga na timu ya Kana Red Devils ya Zambia.

Mbombo ambaye amechezea Azam FC kwa mafanikio amebakiza miezi sita kabla mkataba wake umalizike.

Uongozi wa Azam uko tayari kumuachia nyota huyo mwezi Januari na unasubiria ofa mezaani.

Wakati Mbombo akiwa mlangoni, mazungumzo yamefika pazuri kati ya klabu hiyo na Mshambuliaji Rellants Lusajo ambaye alikuwa Namungo.



## Saadane aitengeneza Stars Algeria

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Taifa Stars leo inashuka dimbani kumenyana na Zanzibar Heroes, Kocha Rabah Saadane ameanza kuiandalia timu hiyo mazingira ya kambi.

Saadane aliyewahi kuwa Kocha wa Algeria yuko nchini humo ambapo jukumu lake la kwanza ni kuandaa kambi ya kikosi hicho ambacho kinakwenda kushiriki michuano ya Mataifa ya Afrika nchini Ivory Coast Januari mwakani.

Rabah anaingia katika kikosi hicho kama Mshauri wa benchi la Ufundi. Inaelewa kuwa hatua ya timu hiyo kuweka kambi nchini Algeria ni mapendekezo ya Kocha huyo mzoefu.

Adel Amrouche bado anaendelea kuwa Kocha Mkuu huku Hemed Morocco akiwa msaidizi wake.

Stars imepeleka majina 53 ya wachezaji kwa ajili ya michuano hiyo huku kukiwa na maingizo mapya ya wachezaji wenye asili ya Tanzania wanaocheza soka nchi za Ulaya.

Mechi ya leo itakuwa sehemu ya kujua nafasi na uwezo wa baadhi ya wachezaji.

